

**Vichwa treni ya umeme vyapokewa**

UKURASA 3

## MAISHA YALIVYO

Mume afunga mwaka akidai talaka kwa fujo

UKURASA 11





UKURASA 17

**Afrika Kusini yaishtaki Israel ICJ, yadai kuna mauaji ya halaiki**





# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 31, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

JUMAPILI

ISSN 0856 • No. 0581541


## RIPOTI MAALUM

# Atokwa vidonda mwili mzima baada kumeza dawa hospitalini

Ni mama wa mtoto wa miezi saba, ahamishiwa hospitali ya kibingwa, madaktari bingwa wabaini... Uk. 2





**Kikongwe ataka uchunguzi madai serikali kupoka shamba lake**

UKURASA 5

## Waziri atoa siku 16 kuamua hatima ya ma-RC, ma-DED

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA SC YAMFUATA MALONGA BRAZAVILLE UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Atokwa vidonda mwili mzima baada kumeza dawa hospitalini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HALIMA Omar Kombo (29), mkazi wa Fundo, Wilaya ya Wete, Pemba, anapitia kipindi kigumu cha maumivu kutokana na mwili wake wote kuharibika na kuwa na vidonda mithili ya mtu aliyeungua moto.

Halima ambaye macho yake jana yalikuwa yanatokwa usaha, amekumbana na adha hiyo baada ya kumeza dawa aina ya Carbamezapine (CPZ) aliyopewa alipokwenda kutibiwa katika Hospitali ya Vitongoji, Pemba.

Kabla ya kukumbwa na tatizo hilo, wazazi wake wanadai alikwenda hospitalini kutibiwa ugonjwa wa kuanguka (kifafa). Amekuwa akisumbuliwa na ugonjwa huo tangu akiwa na umri wa miaka 18, yaani miaka 11 iliyopita na kila alipokwenda hospitalini, ilikuwa kawaida kwa madaktari kumpatia dawa hiyo.

Halima, mama wa watoto wanne (watatu wa kike, mdogo wao wa kike ana umri wa miezi saba), hakuwa na uwezo wa kuzungumza jana alipotembelewa na mwandishi wa habari hizi katika Hospitali Mnazimmoja, akikohamishiwa kwa dharura toka Pemba.

Baba yake, Omar Kombo, mkazi wa Kambini Kichokochwe, Jimbo la Kojani, alibainisha kuwa awali binti yake alikwenda Hospitali ya Vitongoji Desemba 8, mwaka huu, akisumbuliwa na homa na kupatiwa matibabu na kurejea nyumbani.

Kombo ambaye uso wake ulitawaliwa na huzuni, alisimulia kuwa baada ya mwanawe huyo kutumia dawa hizo, alianza kuona mabadiliko mwilini; aliwashwa na kufanya malengelenge mwili mzima huku akiishiwa nguvu.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo, hatua waliyochukua ni kumpeleka mwanawe katika Hospitali ya Micheweni Desemba 19, mwaka huu; huko hali ikazidi kuwa mbaya, ngozi ilibabuka na kufanya vidonda mwili mzima.

"Daktari wa Micheweni aliyetuhudumia alituambia kwamba dawa alizotumia zimemletea madhara, na ndipo tukapata rufani kumpeleka Hospitali ya Abdalla Mzee (Hospitali ya Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba) kwa ajili ya matibabu zaidi," alisema.

Wakiwa katika Hospitali ya Micheweni, Kombo alisema mwanawe alilazwa kwa siku nne kabla ya kuhamishiwa Hospitali ya Abdalla Mzee Desemba 24, mwaka huu, ambako nako alilazwa kwa siku tatu kabla ya kupatiwa rufani kwenda Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja, Unguja Desemba 27 mwaka huu.

Katika hilo, Kombo ana malalamiko kwamba alimsafirisha mgonjwa wake kutoka kisiwani Pemba hadi Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa gharama zake, pia alilipa gharama za daktari aliyesindikiza mgonjwa, kinyume cha maelekezo ya kisera.

"Hali zetu ni maskini na maisha ni magumu. Tuna mgonjwa ambaye anahitaji msaada wetu, lakini pia tulihitajika tugharamie nauli ya daktari ambae tuliongozana naye kutoka Pemba kuja Unguja," alilalamika.

Kombo, baba wa watoto saba - Halima akiwa mtoto wake wa nne, alibainisha kuwa ndugu walichangishana kupata walau nauli ya kumsafirisha daktari.

"Tuliitisha kikao cha familia na kuomba msaada wa gharama za kumsafirisha mgonjwa pamoja na daktari ambapo gharama ya usafiri wa daktari pekee ilikuwa Sh. 120,000," alifafanua.



Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui

**Kabla ya kukumbwa na tatizo hilo, wazazi wake wanadai alikwenda hospitalini kutibiwa ugonjwa wa kuanguka (kifafa). Amekuwa akisumbuliwa na ugonjwa huo tangu akiwa na umri wa miaka 18, yaani miaka 11 iliyopita na kila alipokwenda hospitalini, ilikuwa kawaida kwa madaktari kumpatia dawa hiyo.**

Kombo aliiomba serikali kusaidia kuharakisha matibabu ya mtoto wake, akisisitiza maradhi yanayomkabili kwa sasa yametokana na matumizi ya dawa alizopewa hospitalini.

Pia aliomba serikali kutenga bajeti kwa ajili ya wagonjwa wanaopewa rufani.

Mume wa Halima, Idrisa Ali Shindano, alisema kuwa wakati mke wake anaanza kuugua maradhi hayo yaliyotokana na madhara ya dawa alizomeza, alikikuwa Kizimkazi, Unguja kwa shughuli za uvuvi.

"Niliondoka nyumbani Fundo wakati mke wangu anaumwa homa tu ya kawaida, lakini alikuwa akinipa taarifa kinachoendelea na nililazimika kurudi Pemba baada ya kupata taarifa kwamba mke wangu amelazwa Hospitali ya Mkoani na hali yake haikuwa nzuri," alisema.

Shindano alisema kuwa katika kipindi chote cha ndoa yao, mkewe hakuwahi kupatwa na tatizo hilo, zaidi ya maradhi ya kuanguka yaliyomsumbua kwa zaidi ya mulongo sasa.

Daktari Dhamana wa Hospitali ya Micheweni, Mbwana Shoka, alisema anafahamu kesi ya mgonjwa huyo ambaye alifikishwa hospitalini huko Desemba 19 akiwa katika hali mbaya kiafya.

Alisema uchunguzi wa awali ulibaini mgonjwa huyo amepata madhara baada ya kutumia dawa alizopatiwa katika hospitali ya awali alikopatiwa matibabu.

Alisema wapo baadhi ya watu huwa mzio kwa baadhi ya dawa, lakini haina maana kwamba dawa hizo zina sumu au zimepita muda wake wa matumizi ama hazifai kwa matumizi ya binadamu.

"Kesi kama ya mgonjwa huyu si ya kwanza kutokea, wapo ambao huwa na mzio na dawa na wengine hupata madhara na kupoteza maisha kama hakupata tiba ya haraka na mapema," alisema daktari huyo.

Daktari Dhamana wa Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani, Rashid Saleh Muhammed, alisema walimpokea mgonjwa huyo, akitokea Hospitali ya Micheweni; hali yake ilikuwa mbaya, hivyo kumpa rufani kwenda Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja.

"Si kwamba tulishindwa kumhudumia, bali baadhi ya vifaa vya uchunguzi kama MRI hatuna," alifafanua daktari huyo.

Daktari Bingwa wa Maradhi ya Ngozi, Hospitali ya Mnazi Mmoja, Salama Makame Pandu, alisema walimpokea mgonjwa huyo Desemba 27, mwaka huu na anaendelea kupatiwa matibabu.

Alisema kuwa Halima anasumbuliwa na ugonjwa wa ambao kitabibu unaitwa TEN (Toxic Epidermal Necrolysis).

Dk. Salama alifafanua: "Ni ugonjwa ambao husababisha ngozi kuchubuka, tena sehemu kubwa ya mwili, ikijumuisha mdomo, macho na sehemu za siri. TEN ni aina kali zaidi ya ugonjwa wa Stevens-Johnson. Hali zote mbili husababishwa na mmenyuko wa dawa."

Bingwa huyo alibainisha kuwa takriban watu milioni moja hadi mbili huugua ugonjwa huo kila mwaka duniani kote, akiwa na angalizo kwamba asilimia 20 hadi 60 hufariki dunia.

"Kwa mgonjwa huyu (Halima) dawa zilizomsababishia madhara ni Carbamezapine (CPZ) na upo uwezekano wa kupona na kurejea katika hali yake," alisema daktari huyo.

Alisema dawa zilizomsababishia madhara ni za kutibu na maradhi ya akili ambazo hutumia kutokana na tatizo hilo linalomsumbua.

Bingwa huyo alisema uchunguzi wao umebaini ngozi ya mgonjwa huyo, pia macho vimeathirika kwa asilimia 90.

Dk. Salama aliwataka wananchi kuacha kutumia dawa bila ushauri wa daktari, ingawa Halima alipatiwa dawa hizo hospitalini.

Alisema kuwa kwa sasa mgonjwa huyo anapatiwa matibabu ili kukausha vidonda mwilini, huku akitaja dalili kumi zinazoweza kutokea wiki chache baada ya kuanza kutumia dawa, zikijumuisha homa, maumivu ya mwili, kikohozi, homa na baridi, maumivu ya kichwa na macho kuvimba.

Kuhusu gharama kwa mgonjwa anayepatiwa rufani, Ofisa Mdhamini Wizara ya Afya Pemba, Khamis Bilali Ali, alisema daktari anayembatana na mgonjwa kwa ajili ya kumsafirisha, gharama zote ikiwamo nauli, hulipwa na wizara.

Alisema familia ya mgonjwa anayehitaji kusafirishwa nje ya kisiwa hicho, haitakiwi kulipia gharama hizo.

"Kwa sasa fedha zipo kwa ajili ya nauli ya daktari anayesafirisha mgonjwa nje ya Pemba kwa ajili ya matibabu," alisema.

Ofisa Mdhamini huyo alisema atahakikisha familia hiyo iliyotakiwa kugharamia nauli ya daktari inarejeshewa fedha ilizolipa.

Hata hivyo, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema wizara haina bajeti maalum kwa ajili ya wagonjwa wa rufani, lakini inapotokea hali kama hiyo, hutumia fedha zilizoelekezwa katika maeneo mengine ya wizara.

Kwa mwaka ujao wa fedha (2024/2025), Waziri Mazrui aliahidi serikali itatenga fedha kwa ajili ya kugharamia rufani za wagonjwa, hasa wanaotoka Pemba kwenda Unguja au Tanzania Bara kupata huduma za kibingwa.

# Waziri atoa siku 16 kuamua hatima ya ma-RC, ma-DED

**Na Thobias Mwanakatwe,**
DODOMA

AGIZO la Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI),Mohamed Mchengerwa la kuwataka wakurugenzi wa halmashauri kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya elimu ifikapo leo Desemba 31, mwaka huu, halijatekelezwa. Ujenzi haujakamilika katika baadhi ya mikoa.

Kutokana na hali hiyo, Mchengerwa ametoa siku 16 nyingine za mwisho kwa wakuu wa mikoa kuanzia leo, ujenzi wa madarasa na shule na bweni uwe umekamilika ifikapo Januari 15, mwakani na baada ya hapo hatataka kusikia sababu nyingine zinatolewa na viongozi hao.

Miradi ambayo waziri alitoa agizo hilo ni ile ya ujenzi unaotekelezwa kupitia fedha za Mradi wa Uboreshaji Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara (BOOST) ambayo serikali ilitoa Sh. bilioni 230 katika mikoa yote kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 302 na ujenzi wa miundombinu kwenye Shule za Msingi zilizopo.

Kwa upande wa Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP), serikali ilitoa Sh. bilioni 247.38 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari za kata 228, shule mpya 16 za sekondari za bweni za wasichana na miundombinu katika shule 10 za bweni za wasichana zilizojengwa katika awamu ya kwanza ya 2021/22 na ukarabati wa shule chakavu, ukamilishaji wa maboma ya madarasa, maabara na matundu ya vyoo.

Waziri Mchengerwa akizungumza jana na wakuu wa mikoa kwenye kikao kazi cha kutoa taarifa ya utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya shule za awali, msingi na sekondari kilichofanyika kwa njia ya mtandao, alisema taarifa walizozitoa wakuu wa mikoa, zina matumaini kwa watanzania ingawa bado ukamilishaji miradi katika baadhi ya miradi haujafikia asilimia 100.

"Kwa kuwa wakuu wa mikoa mmeweka ahadi maeneo ambayo mchakato wa ujenzi bado unaendelea na mmesema ikifika Januari 15, 2024, majengo karibu yote yatakuwa yamekamilika na watoto wataendelea na masomo, ninaomba ifikapo tarehe hiyo kwa maelekezo ya Rais hakikisheni majengo yote yawe yamekamilika kama mlivyoahidi," aliagiza.

Alisema baada ya Januari 15, yeye na wasaidizi wake watapita kila mkoa, wilaya na halmashauri kujiridhisha.

Mchengerwa alisema viongozi hao watambue kuwa kuanzia Januari 2024, serikali itaanza kutekeleza kutekeleza mtaala mpya kwa darasa la kwanza na la tatu, hivyo wasimamie suala hilo kama ambavyo sera mpya elimu inasisitiza.

Aliongeza kuwa katika kila miradi inayotekelezwa na serikali, wakuu wa mikoa wahakikishe wakurugenzi wa halmashauri, wahandisi na maofisa ununuzi wanatia saini fomu maalum ili kuthibitisha kwamba fedha wanazozipokea zitakamilisha miradi iliyokusudiwa na kwa wakati husika.

Mchengerwa alisema eneo lingine ni kuhakikisha halmashauri hazivurugi na kwenda kinyume cha utaratibu wa 'force account' katika ujenzi unazozipa mamlaka kamati za ujenzi, ununuzi na mapokezi, hivyo kusababisha kuchelewa kuanza kwa ujenzi.

Pia aliwaagiza wakuu wa mikoa kuhakikisha shule mpya zilizojengwa, hasa za wasichana, zinasajiliwa na zianze mara moja kupokea wanafunzi.

'Natambua ipo mikoa ambayo imekamikisha kwa asilimia 75 hadi 80 lakini hawajaanza kuzisajili kwa ajili ya kupokea wanafunzi," alisema.

Kuhusu chakula, waziri huyo alisema viongozi hao wanapawa kusimamia bajeti za chakula kwa shule zote za bweni ili wanafunzi wawe wanapata chakula.



**HALI MIKOANI**

Wakati wakuu wa mikoa wanawasalisha taarifa ya utekelezaji ujenzi wa miundombinu ya elimu, mikoa ambayo ilikuwa haijakamilisha miradi yote kwa asilimia 100 ni pamoja na Arusha, ambao mkuu wake, John Mongella alisema katika mradi wa BOOST awamu ya kwanza mkoa wake ulipokea Sh. bilioni 3.267.

Alisema ujenzi haujakamilika katika mikondo miwili ya Shule ya Kaitaro iliyopo Halmashauri ya Ngorongoro ambayo inatarajia kukamilika ifikapo wiki ijayo. Ujenzi wa madarasa hayo haujakamilika kwa sababu kata hiyo iko mpakani umbali wa zaidi ya kilometa 100 kutoka makao makuu ya wilaya.

Mongella alisema katika miradi ya SEQUIP, mkoa ulipokea fedha kwa ajili ya miradi 10 katika halmashauri zote za mkoa huo yenye thamani ya Sh. bilioni 4.7 na kwamba minane imeshakamilika na miwili iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro haijakamilika.

Kuhusu ujenzi wa Shule Maalum ya Wasichana inayojengwa Wilaya ya Longido, mkoa ulipata Sh. bilioni tatu. Hadi sasa ujenzi wake umefikia asilimia 68 ya utekelezaji.

Mkoa wa Dar es Salaam nao haujakamilisha miradi yote ya BOOST na SEQUIP kwa asilimia 100. Mkuu wa mkoa huo, Albert Chalamila alisema miradi ya SEQUIP walipokea Sh. bilioni 13 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari 15.

Alisema hadi kufikia Desemba mwaka huu ujenzi wa shule 13 ulikuwa umekamilika kwa asilimia 100 lakini shule mbili ujenzi wake bado unaendelea haujakamilika.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema mkoa umepokea wanafunzi 52,897 ambao wanahitaji madarasa 1,171 lakini yaliyopo ni 1,143, hivyo kuna upungufu wa madarasa 28. Upungufu huo uko katika Wilaya za Nchemba na Chamwino,

Katika mradi wa SEQUIP awamu ya kwanza, mkoa ulipata fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule 10 ambapo kati ya hizo shule sita zimekamilika kwa asilimi 100. Zingine bado.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas alisema ujenzi wa nyumba 28 za walimu ambazo mkoa ulipokea zaidi ya Sh. bilioni 1.8, umetekelezwa; nyumba 10 ziko hatua ya ukamilishaji na nyumba 18 tayari zimeshaanza kukamilika.

Mkoa wa Tabora nao bado haujakamilisha miradi yote ya SEQUIP ambayo serikali ilitoa Sh. bilioni 8.454. Mkuu wake, Balozi Dk.Batilda Buriani alisema ujenzi wa shule mbili ambazo fedha zake zilishatolewa tangu Septemba mwaka huu, haujakamilika. Ifikapo Januari 15 utakuwa umekamilika.

# Vichwa vya treni ya umeme vyapokewa

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Reli Tanzania limepokea vichwa vipya vitatu vya treni za umeme vilivyoundwa na Kampuni ya Hyundai Rotem, mwendo wake ni kilometa 160 kwa saa.

Pia limepokea mabehewa mapya 27 ya abiria yaliyoundwa na Kampuni ya Sung Shin Polling Stock Technoly (SSRST) ya Korea Kusini.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano cha shirika hilo, Jamila Mbarouk, katika taarifa yake jana, alisema serikali kupitia shirika hilo, ilifanya ununuzi wa vichwa vipya 17 na mabehewa 59 ya abiria kwa ajili ya uendeshaji Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR).

Jamila alisema mpaka sasa shirika limepokea vichwa vya treni ya umeme vinne kati ya 17 kutoka kampuni ya Hyundai Rotem na mabehewa 56 kati ya 59 kutoka kampuni ya SSRST.

"Mabehewa matatu yaliyosalia yanatarajiwa kuwasili nchini mwezi Februari mwakani. Vichwa 13 vilivyobaki vinatarajiwa kuwasili kwa awamu ambapo vichwa sita vitawasili mwezi Machi na vichwa saba vitawasili mwezi Aprili, 2024," alisema.


Jamila alisema TRC itaanza kupokea seti ya kwanza kati ya seti 10 za treni za kisasa (EMU) mwezi Machi mwakani, ambapo Mei, Juni, Julai, Septemba watakuwa wakipokea seti mbili kila mwezi na za mwisho zitapokewa Oktoba.

"Mabehewa 27 katika madaraja katika madaraja ya uchumi na biashara. Daraja la biashara ni mabehewa 13, kila behewa lina uwezo wa kubeba abiria 45.

"Mabehewa ya daraja la uchumi ni 14 ambapo kila behewa lina uwezo wa kubeba abiria 78 kwa kuzingatia viwango vya kimataifa kumwezesha abiria kusafiri kwa amani na usalama," alibainisha.

Alisema shirika linaendelea kupokea kwa awamu vitendea kazi kwa ajili ya uendeshaji wa SGR ambapo majaribio ya vitendea kazi hivyo yanaendelea kwa mujibu wa mkataba ili kuhakikisha vinaendana na mifumo ya miundombinu iliyojengwa kabla ya kuanza uendeshaji wa kibiashara.

**KUPOTEA KWA CHETI**



**WILSON DAUD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S. 32740081** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KASHAI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PW/KIB/RB/258719/2021**

RIPOTI MAALUM

## SARAKASI ZA HIFADHI YA SAADANI

# Baraza la Mawaziri laja na uamuzi

**Na Mwandishi Wetu**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipotembelea mashamba ya miwa ya Kampuni ya Bagamoyo Sugar wilayani Bagamoyo, Agosti 18, 2020. **PICHA: MAKTABA**

SARAKASI za Mbuga ya Wanyama Saadani sasa zimelifikia Baraza la Mawaziri:

Mwekezaji wa kiwanda cha chumvi hifadhini amenyimwa kibali cha kutanua mradi wake. Badala yake, eneo la mradi wake limepunguzwa.

Wakazi wa kitongoji cha Kajanjo, wilayani Bagamoyo, wametakiwa kuhama katika maeneo hayo kutokana na kuingilia kwa kiasi kikubwa shughuli za uhifadhi na utalii.

Kwa mujibu wa uamuzi wa baraza hilo uliotangazwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, mwekezaji wa kiwanda cha chumvi hifadhini - Sea Salt Ltd amenyimwa kibali cha kutanua mradi wake. Badala yake, eneo la mradi huo ambalo ni ekari 2,400, limepunguzwa kwa ekari 50.

Kunenge anabainisha kuwa uamuzi wa kuwaondoa wananchi hao katika kitongoji hicho ambacho wenyeji wake wengi ni wavuvi, umetokana na mapendekezo ya Kamati ya Mawaziri Wanane wa Kisekta iliyoshirikiana na timu ya wataalamu kufika katika maeneo yenye migogoro ya ardhi na kutoa mapendekezo ambayo yaliridhiwa na Baraza la Mawaziri kwa utekelezaji.

"Hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chalinze futa kitongoji cha Kajanjo na kuhakikisha wananchi wanahamishwa.

"TANAPA lipeni fidia yenye thamani ya Sh. milioni 287.631 kwa ajili ya mashamba na Sh. milioni 88.806 kwa ajili ya makazi ya kaya 17 zilizokuwapo wakati wa tathmini ya kisheria, na tusione mwananchi yeyote anarudi katika eneo hili," anaelekeza.

Eneo wanakohamishwa wananchi, lina msitu wa mikoko ambayo si tu ni muhimu katika kuzuia mmomonyoko wa udongo, bali pia ilitajwa na wataalamu katika ripoti zetu zilizopita kwamba "ina uwezo mkubwa wa kunyonya hewa ukaa".

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa Kunenge, Baraza la Mawaziri pia limeelekeza Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Pwani afute hati ya miliki ya East Africa Resort kwa kuwa mradi wake umo ndani ya Hifadhi ya Taifa Saadani na haujaendelezwa.

"Haya tunayosema lazima yazingatiwe na hatutegemei kuona tena malumbano, hatutegemei kuona mambo haya yanajirudia," Mkuu wa Mkoa Kunenge anaonya.

Hata hivyo, kilichoamuliwa na Baraza la Mawaziri kinakinzana na ushauri wa wataalamu wa uhifadhi na utalii, akiwamo Profesa wa Mifumo Ikolojia wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Idara ya Mifumo Ikolojia na Uhifadhi, Pantaleo Munishi, aliyeshauri makazi yaondolewe sambamba na kuzuia shughuli za uchimbaji madini na kilimo cha miwa hifadhini Saadani.

**ALICHOJIBIWA CAG**

Wakati Mkuu wa Mkoa Kunenge akitangaza uamuzi huo wa Baraza la Mawaziri, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aliyeibua suala hilo katika ripoti yake ya ukaguzi wa 2020/21, naye ameanika alichojibiwa na serikali.

Katika ripoti ya ukaguzi wa 2021/22 iliyowasilishwa bungeni Aprili 6, mwaka huu, CAG Charles Kichere, anabainisha kuwa amejibiwa kuwa Menejimenti ya TANAPA iliandika barua kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, ikiishauri wizara kwa kushirikiana na wizara inayohusika na madini, kupata msimamo wa serikali kuhusu uendeshaji na umiliki wa kampuni ya Sea Salt.

Anasema ufuatiliaji unafanyika. Menejimenti ya TANAPA inawasiliana na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ili hatua zichukuliwe kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 .

"Nimepokea majibu ya serikali. Nilithibitisha juhudi za serikali kupitia mawasiliano kati ya MNRT (Wizara ya Maliasili na Utalii) na NEMC. Nitafuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao," CAG Kichere anabainisha katika ripoti yake hiyo.

**KILIMO HIFADHINI**

Kuhusu hoja yake ya uendeshaji shughuli za kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari hifadhini Saadani, CAG Kichere anasema alipendekeza serikali na Bodi ya Wadhamini ya TANAPA kutathmini kwa kina athari za shughuli hizo ndani ya hifadhi hiyo na kutafuta njia bora ya kukabiliana na hali hiyo.

Katika hilo, CAG anasema amejibiwa na serikali kwamba Kamati ya Mawaziri Wanane wa Kisekta ilipendekeza kufanyike makubaliano kati ya Hifadhi ya Taifa Saadani na jamii iliyoko huko, ikiwamo Kampuni ya Sukari Bagamoyo; umbali wa mita 200 kati ya 500 kutoka ukingo wa Mto Wami ubaki kwenye eneo la hifadhi na serikali isalimishe mita 300 kwa mwekezaji ambayo ni sehemu ya Hifadhi ya Taifa Saadani.

"Majibu ya Serikali yamepokewa. Nilithibitisha juhudi za Serikali. Nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao," CAG Kichere anaeleza katika ripoti yake.

Katika hilo, hoja ya wataalamu ya TANAPA ni kwamba ili kulinda usalama wa ikolojia ya hifadhini Saadani, mwekezaji wa kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari asalimishe walau eneo la mita 500 kutoka ukingo wa Mto Wami.

Mwekezaji huyo - Bagamoyo Sugar Limited (BSL), kampuni tanzu ya Said Salim Bakhresa (SSBG) amemegewa na serikali hifadhini eneo lenye ukubwa wa hekta 10,000: Namba yake ya usajili ni 3565-1 kwa umiliki wa miaka 66, iliyotolewa Oktoba Mosi, 2016.

Saadani ni hifadhi pekee Afrika Mashariki yenye eneo la nyika na bahari. Iko katikati ya miji ya kihistoria ya Bagamoyo, Pangani na Zanzibar.



Makazi yanayoondolewa hifadhini Saadani.





Mradi wa uzalishaji chumvi uliomo ndani ya Hifadhi ya Taifa Saadani.

HABARI KITAIFA

## NMB yawajaza noti washindi droo kampeni ya Mastabata

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WASHINDI 120 wa kampeni ya Benki ya NMB ya 'Mastabata - Halipoi' wamejinyakulia jumla ya Sh. milioni 24 kama zawadi katika droo yake ya pili ya mwisho wa mwezi huu.

Kampeni hiyo inalenga kuhamasisha matumizi ya kadi na kulipa kwa kuskani QR katika kufanya malipo.

NMB iligawa zawadi hizo juzi wakati wa droo maalum iliyochezeshwa jijini Arusha. Washindi watatu wamefanikiwa kushinda safari ya kwenda na wenza wao Zanzibar itakayogharamiwa usafiri, malazi na chakula, pia posho ya Sh. 200,000.

Droo hiyo ilitoa washindi 100 wa kila wiki waliojishindia kila mmoja Sh. 100,000 na wateja 17 wa mwezi waliojishindia kila mmoja Sh. 500,000.

Akizungumzia droo hiyo wakati wa ugawaji zawadi, Meneja Mwandamizi wa NMB Idara ya Biashara ya Kadi, Manfredy Kayala alisema washindi 120 wa mwezi huu wamegawiwa jumla ya Sh. 24.5 zikiwamo Sh. milioni 10 za washindi 100 wa kila wiki; kila mmoja alijishindia Sh. 100,000.

"Mbali na hao, washindi 17 wa mwezi wamejishindia Sh. 500,000 kila mmoja, huku washindi watatu wakipata safari ya kugharamiwa kwenda Zanzibar na wenza wao na watapewa posho ya Sh. 200,000," alisema Kayala.

Alisema kuwa zawadi hizo ni sehemu ya Sh. milioni 350 walizotenga kutoa kama zawadi zikiwa ni fedha taslimu pamoja na safari za kwenda kupumzika katika visiwa vya Zanzibar na Afrika Kusini.

"Kwa kampeni hii ya awamu ya tano, kuna zaidi ya washindi 1,200 wa kila wiki wanaopata Sh. 100,000 katika kampeni zinazoendelea pamoja na washindi 240 wa papohapo ambao wanapata Sh. 50,000 wanapofungua akaunti au kujibu maswali kadhaa. Hiyo ni pamoja na washindi wa kila mwezi ambao kila mmoja atapata Sh. 500,000," alifafanua.

Alisema kampeni hiyo inalenga kuhamasisha matumizi yasiyotumia fedha taslimu na badala yake watumie kadi, kuskani QR au malipo ya kimtandao ambayo yatapunguza kiwango cha uhalifu unaohusisha watu kuibiwa fedha zao kama ilivyokuwa zamani, pia kukuza uchumi.

Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Praygod Godwin alieleza kuwa promosheni hiyo maalum inatekelezwa na benki hiyo kwa kushirikiana na kitengo cha Mastercard.

Alisema benki hiyo yenye matawi zaidi ya 43 Kanda ya Kaskazini, itaendelea kuja na promosheni mbalimbali ili kuendelea kuwanufaisha wateja wanaotumia huduma zake.

"Ukiwa na Kadi ya NMB, mtu anaweza kufanya miamala wakati wowote na mahali popote ambapo kuna pointi za mauzo (POS)," alisema.

Mmoja wa wateja waliopatiwa zawadi katika droo hiyo, mfanyabiashara Jackline Matowo, alisema alikwenda benki kuweka fedha kwa ajili ya biashara yake, lakini akabahatika kucheza droo ya papohapo na kushinda Sh. 50,000 katika kampeni inayoendelea.

"NMB wamefanya kampeni nzuri sana, inahamasisha wateja kuendelea kutumia huduma za kifedha kidigitali kwa kutambua zawadi hizi, lakini inaleta usalama wa fedha zetu na zaidi inasaidia nchi kujua maendeleo yake kiuchumi," alisema.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko ambaye ni Mbunge wa Bukombe, akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella (kushoto) kabla ya kuzungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara kwenye kijiji cha Bukombe, kata ya Bukombe, wilaya ya Bukombe mkoani Geita ikiwa ni sehemu ya ziara yake jimboni Bukombe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

LICHA YA TAMKO LA RC...

# Kikongwe ataka uchunguzi serikali kupoka shamba lake

**Na Thobias Mwanakatwe**

SINTOFAHAMU imeendelea kugubika shamba la kikongwe Zaina Kipanga (88), anayedai kuporwa eneo na serikali, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba amesema shamba hilo ni mali ya serikali.

Wiki iliyopita Nipashe iliripoti kuhusu madai ya kikongwe huyu ambaye alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati mgogoro huo wa shamba lenye ekari 12 baina yake na Serikali ya Kijiji cha Kwamsisi, mkoani Tanga.

Zaina alidai kuwa uongozi wa kijiji chicho umefyeka mahindi shambani huko aliyopanda msimu huu wa mvua kutokana na mgogoro huo.

Baada ya taarifa hiyo kuripotiwa na Nipashe, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari Jumanne ya wiki hii, alisema anaitambua familia hiyo.

Alisema familia ya marehemu Omary Kipanga (aliyekuwa mume wa kikongwe huyo), imekuwa inalalamika kuhusu ardhi ya Kwamsisi kwa muda mrefu.

Alisema eneo linalolalamikiwa, Halmashauri ya Mji wa Korogwe ilipanga kuanzisha mnada wa mifugo katika mwaka huu wa fedha ambapo mwezi Agosti, kijiji kilifanya harambee ya kwenda kusafisha eneo hilo.

"Mwaka 2021, mlalamikaji alipeleka malalamiko Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tanga, utatuzi ulifanyika kwa kufuata taratibu zote na hivyo hitimisho lilitolewa kuwa eneo lenye mgogoro ni mali ya Serikali ya Kijiji cha Kwamsisi.

"Hivyo, familia hiyo ilishauriwa kuomba eneo kwenye serikali ya kijiji kama ambavyo wengine huomba kwa ajili ya kilimo, jambo ambalo familia hiyo haikufanya," alisema.

Kindamba alisema upo ushahidi tosha kwamba toka mwaka 1978, serikali iliweka miundombinu kadhaa katika eneo hilo likiwamo josho la serikali. Pia vipo vyoo ambavyo vilijengwa muda mrefu katika eneo hilo.

"Familia ya Omary Kipanga imekuwa inalalamika juu ya ardhi ya Kwamsisi kwa muda mrefu. Hata hivyo, hakuna mahindi wala mazao yao yaliyoharibiwa na Kijiji cha Kwamsisi au Halmashauri ya Korogwe TC katika mwaka huu," alisema.

**KIKONGWE ALALAMA**

Pamoja na majibu hayo ya Mkuu wa Mkoa, kikongwe huyo amemwomba Rais Samia kuunda tume kuchunguza suala hilo ili haki itendeke.

Zaina alisema harambee ya kusafisha shamba ambayo Mkuu wa Mkoa ameeleza katika taarifa yake ndio siku kijiji hicho kilipokwenda kufyeka mazao katika shamba lake hilo.

Katika maelezo yake awali, kikongwe huyo alidai viongozi wa wilaya wameshindwa kumsaidia, hali aliyoiita ni njama za makusudi za kutaka kupoka shamba hilo.

Kikongwe huyo alisema shamba hilo ambalo sasa amepigwa marufuku kuingia humo, yeye na mumewe Waziri Kipanga, walikuwa wanalima tangu wakati wa Operesheni Vijiji iliyofanyika miaka ya 1970. Operesheni hiyo ilikuwa agizo la Rais wa wakati huo, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaelekeza kuwa kila mtu ana haki ya kumiliki mali na hifadhi ya mali yake, ikiwamo ardhi.

Pia inaelekezwa kisheria kwamba ni marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au madhumuni mengine yoyote bila kulipwa fidia kamili ya haki na mapema kwa mujibu wa kifungu cha 3(1)(g) cha Sheria ya Ardhi na. 4 ya Mwaka 1999, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Kifungu cha 3(1)(g) cha Sheria ya Ardhi kinaeleza ardhi inayomilikiwa na mtu binafsi ni marufuku kutwaliwa na serikali au kwa namna yoyote kwa manufaa ya umma isipokuwa ulipaji fidia umefanyika kikamilifu kwa haki na mapema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mwaka 2024 watu wafanye kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo

**LEO** ni tamati ya mwaka 2023. Kumalizika kwa mwaka huu ni kuanza kwa mwaka mpya wa 2024 ambao kiujumla utakuwa na matukio mengi yakiwamo ya kisiasa kama vile kutimiza miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar na pia miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Unguja uliozaa taifa la Tanzania.

Pamoja na matukio hayo makubwa ambayo huadhimishwa kila mwaka lakini kwa mwaka 2024 yatakuwa makubwa na ya kihistoria, pia ni mwaka ambao Watanzania watashuhudia mabadiliko mbalimbali ya sheria ndani ya bunge hasa Sheria ya Uchaguzi na ile ya Vyama vya Siasa. Aidha, ni mwaka ambao Watanzania watafanya uchaguzi wa serikali za mitaa kwa maana ya uchaguzi wa viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa.

Licha ya kuwapo kwa matukio hayo makubwa kisiasa, Watanzania leo usiku, hasa wale Wakristo, watakuwa katika nyumba za ibada kwa ajili ya ibada ya mkesha wa Mwaka Mpya na pia kesho watakuwa na ibada ya Mwaka Mpya. Hata hivyo, kama ilivyo desturi katika kusherehekea Mwaka Mpya, wako baadhi ya watu ambao huenda katika nyumba za starehe kwa ajili ya kufurahia kuumaliza mwaka unaoisha na kuukaribisha mwaka mpya.

Katika kusherehekea huko, miongoni mwa watu hutumia vinywaji kupita kiasi na kulewa chakari na wale wenye vyombo vya moto huendesha kwa fujo kutokana na matumizi ya vileo kwa kiasi kikubwa. Matokeo ya yote hayo ni baadhi ya watu kupoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa kudumu.

Ni vyema Watanzania wakajenga utamaduni wa kupanga malengo ya kuyatekeleza kwa kufanya kazi ili kujiletea maendeleo. Katika hili ni watu wachache ambao hupanga mipango jumuishi ya kifamilia kwa ajili ya kuinua kipato na uchumi wa familia. Kabla ya kufanya hivyo, hufanya tathmini ya mipango ya mwaka unaomalizika kwa kuangalia mafanikio na changamoto katika yale ambayo hawakuyatekeleza.

Watanzania wanapaswa kujenga utamaduni na desturi ya kupanga mambo ya kufanya katika mwaka mzima badala ya kuendelea kuishi kwa mazoea kuwa riziki itapatikana kwa neema za Mungu. Ni kweli Mungu anasaidia watu wake kujipatia riziki lakini bila juhudi ni bure.

Watu wanatakiwa wafanye kazi kwa bidii na hata katika maandiko matakatifu Mungu anawaagiza waja wake kuwa watakula kwa jasho lao, hivyo ni lazima kufanya kazi ili kujipatia riziki. Huu ni ukweli ulio wazi kwamba tofauti za wanadamu katika mafanikio ni kutokana na kufanya kazi, hivyo yule anayeweka juhudi zaidi kutekeleza malengo yake au kufanya kazi anakuwa na nafasi kubwa ya kupata mafanikio kuliko mwingine.

Hivi sasa kumezuka mtindo wa vijana kulalamika kuwa hakuna ajira, hivyo kuamua kukaa vijiweni na kucheza kamari ilhali kuna fursa nyingi ambazo zinaweza kutumika kujiletea maendeleo. Kwa mantiki hiyo, vijana ni lazima wabadilike na kujibidiisha katika kazi hasa za kujiajiri ili kupata riziki na maendeleo kwa ujumla.

Kwa mantiki hiyo, rai yetu ni kwamba mwaka 2024 uwe wa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kuleta tija na maendeleo kwa mtu mmoja, familia, jamii na taifa kwa ujumla. Watu watumie muda mwingi kufanya kazi badala ya kupiga soga sehemu za kazi, kubishana na kulumbana kwa mambo yasiyo na tija pamoja na kuacha kunung'unika katika mambo mbalimbali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwaka 2023 ulikuwa wa vyama vya siasa kutoka kifungoni

Na Sabato Kasika

**LEO** ni siku ya mwisho ya safari ya miezi 12 ya 2023 ambayo imekuwa na milima na mabonde, kutokana na kwamba baadhi ya watu wametangulia mbele ya haki na wengine wakiwa vitandani hawajiwezi.

Lakini pamoja na hayo, kinachotakiwa ni kumshukuru Mungu kwa kila jambo, liwe jema au baya, kwa kuzingatia kwamba ndiye anayeruhusu hayo yote, huku akiwapa wengine nafasi ya kuuona mwaka mpya.

Safari ya mwaka 2023 inapohitimishwa, ni wazi kuna matukio mengi yaliyotokea tangu Januari hadi leo, lakini ninapenda kukumbushia moja katika siasa, ambalo ninaamini lilikuwa ni faraja kwa wanasiasa.

Januari 3, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alikutana na viongozi wa vyama vya siasa Ikulu jijini Dar es Salaam na kutangaza kuondoa marufuku ya mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa.

Rais aliruhusu rasmi mikutano hiyo ambayo tayari vyama vimekuwa vikiifanya maeneo mbalimbali nchini. Hivyo, mwaka 2023 unaofikia kilele chake leo, ulikuwa wa vyama hasa vya upinzani kutoka kifungoni.

Ikumbukwe, ruhusa hiyo na kuhakikishiwa usalama, vilimfanya mwanasiasa na mbunge wa zamani wa Singida Mashariki (CHADEMA), Tundu Lissu, aliyekuwa akiishi Ubelgiji, kurejea nyumbani.

Mwanasiasa huyo alirejea Januari 25 baada ya takriban miaka mitano akiishi uhamishoni na sasa anaendelea na shughuli za kisiasa kama kawaida na viongozi wenzake wa CHADEMA.

Awali, Lissu alianza kuishi uhamishoni nchini Ubelgiji baada ya kuondoka Kenya, Januari 2018 alipokuwa akipatiwa matibabu baada ya kunusurika shambulio la mauaji Septemba 7, 2017 jijini Dodoma.

Lakini alirudi nchini kwa mara ya kwanza Julai 2020, ili kushiriki uchaguzi mkuu akiwania nafasi ya urais. Baada ya uchaguzi huo uliofanyika Oktoba, 2020 kuisha, alilazimika kukimbilia ubalozi wa Ujerumani nchini kupata hifadhi.

Sababu ya kukimbilia katika ubalozi huo, alieleza kuwa ni kutokana na kile alichodai usalama wake kuwa hatarini. Ndipo akafanikiwa kuondoka na kurudi Ubelgiji hadi Januari 25, mwaka huu, aliporejea.

Kurejea kwa Lissu kunatokana na Rais Samia Suluhu Hassan kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa baada ya marufuku ya miaka zaidi ya sita iliyowekwa na mtangulizi wake, hayati John Magufuli.

Mazingira hayo yalimfanya mwanasiasa huyo machachari kuweka wazi kuwa hawezi kuendelea kuishi uhamishoni bila ukomo na kuamua kuchukua hatua ya kurejea nyumbani kuendelea na harakati za kisiasa.

Kwa sasa Lissu anayesifika kwa ukosoaji dhidi ya serikali anaendelea na harakati za kudai katiba mpya na tume huru ya uchaguzi kwa kushirikiana na wanachama wenzake wa CHADEMA.

Hatua ya mwanasiasa huyo kurejea, imechangia kuwapo kwa amsha amsha ya kisiasa na hasa, katika mikutano ya hadhara ambayo ameifanya maeneo mbalimbali tangu arejee nchini.

Miongoni mwa amsha amsha hizo ni sakata la mkataba wa bandari ambalo yeye na viongozi wenzake wa CHADEMA walilivalia njuga na kuhamasisha wananchi kukataa bandari kupewa wawekezaji.

Hivyo, 2023 katika siasa, ni mwaka wa Lissu kurejea baada ya kuishi uhamishoni kwa zaidi ya miaka mitano na kuendeleza harakati za kisiasa kuelekea uchaguzi wa 2024 na 2025. Lakini pia ni mwaka ambao Rais Samia aliweka mazingira mazuri ya kuendesha shughuli za kisiasa baada ya kuondoa marufuku ya mikutano ya hadhara, ambayo iliwanyima nafasi wapinzani kujinadi kwa wananchi.

Pamoja na hayo, Juni mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, alitoa kauli kwamba Rais Samia ametengeneza mazingira mazuri ya kisiasa na kuifanya nchi kuwa salama, hivyo hakuna sababu ya viongozi wa kisiasa wakiwamo wa chama cha CHADEMA walioko uhamishoni kutorejea nchini.

Kauli hiyo iliongeza matumaini na kumfanya mbunge wa zamani wa Arusha Mjini, Godbless Lema naye kurejea nchini, kwani serikali ilishawahakikishia usalama viongozi wa upinzani na wafuasi wao.

Siasa za Tanzania zilichukua sura ile iliyokuwapo kabla ya mwaka 2016 ambazo ni za ushindani kupitia mikutano ya hadhara ambayo imevifanya vyama kujiongezea wanachama na mashabiki.

Hivyo, ukiona mtu anayefukuzwa anakimbia sana, ni vyema pia kumsifia anayemfukuza. Nina maana kwamba tunavyoona siasa za Tanzania zinavyoendelea kustawi, hatuna budi kumsifia aliyechangia zistawi.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Mwaka 2024 ni mageuzi ya kidemokrasia Tanzania



Pascal Mayalla

LEO Desemba 31, tunauaga mwaka 2023 na kuukaribisha mwaka mpya wa 2024. Kwa mantiki hiyo, naomba nianze makala yangu hii ya kwa kuwatakia Heri ya Mwaka Mpya 2024 kwa rai moja tu kwamba mwaka 2024 ni wa mageuzi ya kidemokrasia Tanzania.

Ni mwaka ambao tunabadili sheria yetu ya uchaguzi iwe bora zaidi. Tunabadili Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kuunda Tume Huru na Shirikishi ya Uchaguzi, hivyo tunapaswa kufanya mabadiliko madogo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzana ili kuuondoa ubatili fulani ndani ya katiba yetu.

Nimegundua sisi Watanzania, kwa jina letu maarufu la Wabongo ni watu wa maneno maneno mengi, kulalamika sana na kulialia kwingi. Lakini tukija kwenye matendo na kuchukua hatua, kusema ukweli kabisa, sisi ni wazito wa kufanya vitendo na kuchukua hatua lakini kwenye awamu hii ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliunda kikosi kazi, kikatoa mapendekezo, miswada ya sheria imeishatungwa na kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza, sasa inajadiliwa na wadau na kutungwa kuwa sheria, ila lile kubwa kuliko la ubatili wa katiba yetu, lenyewe bado halipo na hilo sasa ndilo mimi nasimama nalo mwaka 2024.

Wengi huuanza mwaka mpya kwa kuweka malengo ya mwaka kwamba mwaka huu nitafanya hili na lile lakini katika kupanga hayo malengo, si wengi hufanya mapitio ya mwaka ulioisha kwamba walipanga kufanya nini, wametekeleza nini, wamefanikiwa nini na wamekwama nini, ili baadhi ya yale malengo ya mwaka uliopita, ambayo hayakufanikiwa, yabebwe katika mwaka unaofuata au kama hayabebeki yafutwe, na si kila mwaka unakuja na malengo mapya, mwisho wa mwaka hufanyi tathmini wala mapitio ya mwaka ulioisha, kisha unakuja na mengine mapya!, mwisho wa siku, unakuwa huwezi kupima mafanikio yako.

Katiba ya nchi ndiyo Biblia na ndio Msahafu wa uendeshaji wa nchi yetu. Kama ilivyo Ikulu ni mahali patakatifu. Katiba ni kitabu kitakatifu kwa nchi yetu kama vilivyo vitabu vitakatifu vya Biblia Takatifu kwa Wakristo na Quran Tukufu kwa Waislamu. Hii ndio sheria mama ya uendeshaji wa nchi yetu.

Tofauti pekee kati ya Biblia, Msahafu na Katiba ni kwamba Msahafu haubadiliki, Katiba inaweza kubadilishwa lakini mabadiliko yoyote ya katiba, lazima yawe ni mabadiliko halali ya haki. Katiba ndiyo sheria kuu kuliko zote za nchi. Viongozi wetu wakishachaguliwa, tunawaapisha kwa mujibu wa Katiba, wanaapa kuilinda na kuitetea katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ikitokea hata Rais amekiuka Katiba, anaondolewa madarakani.

Sheria yoyote ikitungwa, ikiwa ni kinyume cha katiba, sheria hiyo inahesabika ni batili (null and void). Anayebatilisha sheria batili sio Mahakama Kuu, ni katiba yenyewe, kazi ya Mahakama Kuu ni kuthibitisha tuu huo ubatili na tangu unapothibitika, ubatili huo unakuwa umebatilika.

Tanzania kuna kuna sheria ya uchaguzi ambayo ni batili, kwa kwenda kinyume cha katiba kisha ubatili huo, ukaja kuchomekewa kiubatili ndani ya katiba yetu, licha ya Mahakama Kuu kuitangaza sheria hiyo ni batili na uchomekeaji ubatili huo kwenye katiba pia ni batili, kifungu hicho bado kipo na sheria hiyo bado ipo. Mabadiliko ya sheria ya uchaguzi tunayokwenda kuyafanya hayagusi mabadiliko ya katiba, hivyo ubatili huo bado upo.

Sisi Watanzania tuna fani mbalimbali, kuna wenzetu kazi yao ni kufikiri na kupanga mikakati, hawa wanaitwa 'think tanks'. Kuna wenzetu ni viongozi, kazi yao ni kutuongoza na kuna wenzetu ni watendakazi, kazi yao ni kutenda kazi kwa kutumia nguvu zao. Kuna wengine tukiwamo sisi waandishi wa habari na vyombo vya habari, wa kiasili, yaani "traditional media" kazi zetu kuu ni kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha, hatuna kutenda. Tumegawanyika makundi mawili, waandishi wa habari wa vyombo vya utangazaji ambao kazi yao ni kutangaza na kuongea tu, hakuna kutenda lolote. Na waandishi wa habari wa magazeti kazi yao ni kuandika tuu hakuna kutenda lolote.

Lakini ujio wa mapinduzi ya kidigitali kwenye dunia yetu na ujio wa mitandao ya kijamii. Haya makundi mawili ya vyombo vya habari, yaani broadcast media na print media, yameunganishwa na mtandao wa jamii, hivyo kule kwenye mtandao hakuna 'print' peke yake wala broadcast peke yake. Vyombo vya utangazaji vina kurasa zake za mitandao ya kijamii navyo sasa vinaandika. Mtu unaweza kusoma magazeti, navyo kwenye kurasa zake, vinatangaza na kuweka magazeti mtandao.

Siku hizi kupata habari, kuangalia TV au kusoma gazeti, si lazima ukae nyumbani uwashe TV uangalie habari, ukijisajili tuu na mtandao fulani, wanaita ku 'subscribe', unaletewa tu habari kila inapotokea, hivyo mtu hana tena haja kusubiria taarifa ya habari saa mbili usiku, kila tukio linapotokea linatangazwa 'live', hivyo kufikia ule muda wa habari, kila kilichotokea, watu wanakijua, magazeti ya kesho yake, sisi tunayasoma leo, maana kwenye kurasa zao za mitandao, kila habari, inachapishwa pale pale inapotokea.

Ujio huu wa mitandao ya jamii, umemfanya sasa kila mtu kuwa ni mwandishi wa habari, kila mtu sasa ni mtangazaji, hali inayopelekea hata sisi ambao ni watangazaji wa kweli wa kusomea hii kazi, kujikuta hatufui dafu mbele ya watangazaji vijana wa kisasa kwenye mitandao ya jamii, hivyo ukiwauliza vijana wa kisasa, unamjua Pasco Mayalla?, atakuuliza,

**Kwa heri 2023, karibu 2024.**
**Heri ya Mwaka Mpya!.**
**Paskali. 0784 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania uchaguzi ujao tusiangalie makunyanzi



Na Joseph Kulangwa

MSIJISAHAULISHE jamani, leo ni Desemba 31, mwisho kabisa wa mwaka 2023. Kesho tutakuwa tunatakiana heri ya mwaka mpya na kuanza kusahau yaliyopita tukiganga yajayo, huku yaliyotokea jana tukiyaita ya mwaka jana.

Kwa hiyo tutakiane heri ya mwaka mpya ifikapo kesho, huku tukimshukuru Rabuka kwa alivyotulinda mpaka kuuona mwaka 2024 lakini pia tukimwomba kama alivyotusaidia mwaka unaopita, aendelee hivyo hivyo na mwaka huo ujao kesho.

Ni mengi mazuri na mabaya tumepitia kama binadamu lakini pia kama Watanzania, tumesigana na kupatana kisiasa, kiuchumi lakini pia kijamii bila kuacha kimichezo na hata kimapenzi, lakini inshallah, huenda kesho tukaiona.

Kumbukeni kuwa mwaka unaoanza kesho utakuwa na pilikapilika nyingi hususan katika masuala ya kisiasa, ni mwaka wa uchaguzi wa serikali za mitaa, tunachagua viongozi kuanzia vijijini mpaka mitaani, huku tukijipanga kwa uchaguzi mkuu mwakani.

Huu mwaka ni sawa na yale mapambano ya awali ya masumbwi ya kina 'Mandonga', kusubiri mapambano makubwa yanayohusisha kina Ibra Class, Kiduku, Dulla Mbabe, Mfaume na wengineo. Uchaguzi wa Serikali za mitaa ni mapambano ya awali.

Bila shaka kila mmoja atakuwa anajiandaa kupata kiongozi wake mtaani na kuangalia jinsi matokeo ya mwakani yatakavyoathiri ya 2025 ambayo ndiyo huwa makubwa yanayotikisa nchi, kwani huamua mustakabali wa taifa.

Ikumbukwe kuwa viongozi wa mitaa ndio tunaoishi nao na kama tukikosea kuchagua, basi itakuwa inakula kwetu, kwa sababu tutakuwa pia tunakosea katika uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na Rais. Mwakani tutapokea shikamoo nyingi kutoka kwa wanaotuzidi umri kwa kuwa tu watakuwa wanajishusha kwa nia ya kuomba kura kutoka kwa rika tofauti za watu husussan wenye sifa ya kupiga kura.

Utakuwa mwaka wa kupokea zawadi na takrima nyingi kutoka kwa hata tusiwajua, kwa sababu tu nyuma ya pazia kuna ulaji unatafutwa na wakarimu hao na watoa zawadi.

Hali kama hii tulishaizoea huko nyuma, ambako tumekuwa tukipofushwa na vijizawadi na vitakrima fulani vya kujichekesha na kujikuta tukichagua si viongozi bora bali bora viongozi wa kuziba tu mapengo.

Tunajikuta tukichagua watu wanaojirahisi kwetu, lakini wakishapata nafasi walizoomba, hutugeuka na kuangalia zaidi wa karibu yao hususan ndugu, jamaa, marafiki na familia zao, nasi kutuacha tukigugumia kwa mateso.

Kwa kifupi, ieleweke tu kuwa uongozi Afrika na hasa nchini, ni njia ya watu kujitafutia ukwasi, na ndiyo sababu hutumika hila na njia nzuri na mbaya za kuhakikisha watu au mtu anachaguliwa kushika nafasi fulani kwa sababu ya hulua.

Uchafu mwingi katika mchakato huo wa uchaguzi, hufanywa na vyama vya siasa ambavyo ndivyo hutoa tiketi za watu kugombea, kwani rafu hupigwa dhidi ya wasio na nguvu na kudondoshwa, ili tu kupisha wenye nguvu. Huko nyuma tulipata kushuhudia wakubwa wakilazimisha watu wao kugombea uongozi, na kuwasimamia hata kuhakikisha wanapata nafasi hizo na hatimaye kushindwa kuhudumia wananchi waliowachagua kwa mbinde.

Tumeshuhudia watoto, wake, wajomba, wadogo, mashangazi, dada na hata mama za viongozi, wakihakikishiwa nafasi za uongozi ili mradi tu kudumisha ufalme katika familia hata kama wapewao dhamana hawana sifa wala uwezo.

Yote hayo yanafanyika ili kuhakikisha kwamba 'familia yangu' haitetereki kiuchumi, ili mradi ina mahali penye mrija wa kuingizia kipato ambako huko ni kwenye siasa.

Hivyo Watanzania kama safari hii katika uchaguzi wa serikali za mitaa tutakaa sawa na kuelewa nini tunakitaka kwa maslahi yetu kama Taifa, hatutafanya makosa ya kusikiliza wenye nacho, ili tu kuwachagulia watu wao.

Tukikosea katika uchaguzi ujao, tutakosea uchaguzi wa 2025 kwa madiwani, wabunge na hata Rais. Tukisikiliza kauli za ukichagua mpinzani hatutapeleka maendeleo tukachagua wa chama tawala wasio na uwezo, tutaula wa chuya.

Mwakani na mwaka 2025, tusiangalie sura ya mtu, tusiangalie chama cha mtu, tusiangalie itikadi ya mtu, bali tuangalie sifa na uwezo wa mtu katika kutuwakilisha, kutusimamia na kutuongoza.

Tumeshuhudia madiwani na wabunge ambao baada ya kuchaguliwa, hutoweka na wasipatikane hata kwa simu na kuja kuonekana karibu na uchaguzi wakisheheni uongo na ahadi hewa.

Mwaka ujao na mwaka 2025 tutashuhudia chawa wengi wakijinasibu kuwa karibu na wakubwa, wakiwasifia kwa kila hali na kila jambo kwa matumaini ya kupewa nafasi za kugombea uongozi mitaani na hata bungeni na hatimaye serikalini. Tumeyashuhudia haya!

Kujikomba kwa namna ya uchawa, kumefanya tumepata viongozi dhaifu wanaoishi kwa mapambio ya sifa, huku wakishindwa kusaidia wananchi wanaowaongoza, na matokeo yake ni kilio kila kona ya nchi. Watanzania tunapita kipindi kigumu sana, uchaguzi ujao tufanye kweli bila kigugumizi. Mungu yuko nasi. Amina!

# Makamu wa Rais ataja fursa ujenzi wa barabara Pemba

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ujenzi wa barabara ya Kipapo-Mgelema, Mkoa wa Kusini Pemba utaondoa changamoto ya usafiri kwa wananchi na kukuza uchumi.

Katika ufunguzi wa barabara hiyo jana wilayani Chakechake, Pemba, ikiwa ni shamrashamra za sherehe za Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Othman aliwataka wananchi kutumia miundombinu hiyo kwa manufaa ya kiuchumi.

Alisema kutokana na juhudi za serikali kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu ya kwanza yenye urefu wa kilometa 5.3, kutawawezesha wakulima kusafirisha mazao yao kwa urahisi na kuwapo unafuu wa gharama za bidhaa kwa wananchi wa maeneo hayo.

Othman alisema hatua hiyo pia itawasaidia wananchi kuzifikia kwa wepesi huduma mbalimbali zikiwamo za elimu na afya sambamba na unafuu wa usafiri wa abiria.

Kiongozi huyo aliwataka wananchi kutumia barabara hiyo kwa maslahi ya kiuchumi ili kusaidia kukuza maendeleo yao, hasa katika sekta za kilimo na biashara.

Pia alikumbusha suala la utunzaji mazingira kwa kuhakikisha wanapanda miti ya uchumi na matunda kwa kuwa kufanya hivyo kutawainua kiuchumi.

Alisema ujenzi wa barabara ni gharama kubwa ambapo kwa makisio ya chini kilometa moja hujengwa kwa wastani wa Dola za Marekani 600,000 ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 1.3.

Aliitaka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar kuhakikisha wanatoa elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya barabara hiyo.

Makamu wa Rais alisema serikali kwa kuthamini wananchi wake, tayari imetumia zaidi ya Sh. milioni 572 kulipa fidia wananchi ambao mashamba na nyumba zao zimeathirika kutokana na kupitia na ujenzi wa barabara hiyo.

Kuhusu udhalilishaji, Othman aliwataka wananchi wote kushiriki katika mapambano hayo, pia kuacha tabia iliyozuka kwa baadhi ya watu kulifanya suala la udhalilishaji kama biashara na kuwabambika kesi wananchi wasiohusika na masuala hayo.

Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar, Dk. Khalid Salum Abdalla, alisema chachu ya maendeleo ya kiuchumi ni kuwapo miundombinu bora ikiwamo ya barabara na viwanja vya ndege.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa inatilia mkazo suala hilo katika jitihada za kukuza uchumi na maendeleo kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Matar Zahor Masoud, alisema ujenzi wa barabara hiyo ni hatua muhimu ya wananchi wa eneo hilo kuwezeshwa kiuchumi.

Masoud alisema zaidi ya nusu ya karafuu inayozalishwa Pemba hutoka katika Mkoa wa Kusini na eneo hilo likiwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa zao hilo.

Katibu Mkuu katika wizara hiyo, Khadija Khamis Rajab, alisema barabara hiyo ina uwezo wa kupitisha magari yenye uzito usiozidi tani 10.



Mweneykiti wa Umoja wa Vijana wa CCM taifa Mohamed Ali Kawaida pamoja na Kiongozi Mkuu wa Matembezi Machano Ali Machano na Maafisa usafirishaji wakiendesha pikipiki za bodaboda mara baada ya kuzungumza nao ikiwa ni ishara ya ushirikiano na kuadhimisha miaka 60 Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: IKULU**

## TAPSEA yawapa msaada wanafunzi walioathiriwa maporomoko ya Hanang

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Waandishi Waendesha Ofisi (TAPSEA) Mkoa wa Dodoma kimetoa pole na msaada wa vifaa mbalimbali kwa waathirika wa maporomoko ya tope, mawe na magogo yaliyotokea wilayani Hanang, mkoani Manyara mwanzoni mwa mwezi.

Msaada huo ambao ni mchango wa TAPSEA Mkoa wa Dodoma unajumuisha vifaa vya shule yakiwamo madaftari, sare za shule, kalamu na nguo, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni tano.

Mwakilishi wa chama hicho, Conjeta Chambila, alisema wameona umuhimu wa kuchangishana kwa lengo la kusaidia wenzao.

Chambila alimshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Balozi Aisha Amour kwa kuwawezesha usafiri kutoka Dodoma hadi mkoani Manyara.

"Tunamshukuru sana Katibu Mkuu wa Ujenzi kwa kuweza kutukusanya pamoja na kutuwezesha kutupa usafiri pamoja na kwamba tunatoka ofisi mbalimbali," a;osema Chambila.

Chama hicho pia kimetoa wito kwa waandishi waendesha ofisi wengine wa mikoa ya karibu kuwasaidia waathirika hao ambao walipoteza ndugu na mali zao kutokana na maafa hayo.

Katibu Tawala Mkoa wa Manyara, Athuman Likeyekeye, aliwashukuru waandishi waendesha ofisi hao kwa upendo wao wa kuwasaidia waathirika hao katika kipindi hiki.

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kwa kushirikiana na wakuu wa mikoa na wilaya, inaendelea kupokea misaada mbalimbali kwa ajili ya waathirika wa maporomoko hayo yaliyotolea Desemba 3, mwaka huu na kusababisha vifo vya watu 89 na uharibifu wa miundombinu na makazi.

# TFS yampongeza Rais mikakati utunzaji misitu

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Magharibi, mkoani Tabora, umempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada za serikali yake kuhakikisha nchi inalinda rasilimali za misitu na vyanzo vya maji kwa maslahi ya taifa.

Kamanda wa TFS, Kanda ya Magharibi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Ebrantino Mgiye, aliyasema hayo juzi ofisini kwake, akiitaja ni hatua hiyo ni muhimu kwa mustakabali wa taifa.

Kamishna Mgiye alisema hatua hiyo ya Rais Samia ni mpango mzuri katika kupambana na majanga asilia ya ardhi na kusaidia rasilimali misitu kuendelea kunyonya hewa ukaa na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Kampeni ya upandaji miti ilianza mwaka 2020 kwa lengo la kupambana na tatizo la ukataji miti ovyo kwa kurejesha uoto wa asili katika mikoa yote nchini.

"Kampeni hii inaitaka kila halmashauri kupanda miti zaidi milioni moja na itasaidia pia upatikanaji mazao ya misitu na kulinda nyanzo vya maji na kukinga nchi dhidi ya majanga," alisema.

Kamishna Mgiye alisema mkoa huo pia unatarajiwa kuanza utekelezaji kampeni hiyo mwakani kuelekea kampeni ya siku ya mazingira ya misitu duniani ambayo husherehekewa Machi Mosi. "Tunawashukuru waandishi wa habari kwa kuwa mstari wa mbele katika kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi wa misitu na mazingira na kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kutosha," alisema.

Aliwataka wananchi mkoani hapa na taasisi mbalimbali za serikali na kijamii kuhakikisha wanajitokeza kwa wingi kuchukua miti inayotolewa bila malipo na wakala huo kwa ajili ya kuipanda katika maeneo yao.

JUMAPILI DESEMBA 31, 2023
Nipashe

# MAISHA


Baba, Mama na Mwana




# FURAHIA ‘SIXPACK’ ukivaa mavazi haya...

Ukurasa 13

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | M | E | C | H | I |
| A | ■ | ■ | ■ | H | ■ | M |
| S | ■ | L | O | A | ■ | B |
| H | A | O | ■ | M | E | I |
| I | ■ | A | N | A | ■ | S |
| M | ■ | N | ■ | ■ | ■ | H |
| O | N | A | N | A | ■ | A |

## AMSHA AKILI


HAYA, NJIA GANI TUPITE KUTOKA ALAMA A HADI B?




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MKE, MBA, GIA, ZEE, UTORO, NDEGE, ELEZA, MAMBO, KUNGURU, ENDESHA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



**Alichokifanya daktari**

MTOTO Juma alikuwa akimsaidia mama yake kulima bustani ya mboga pembeni ya nyumba yao. Wakati wanalima Juma alianza kumuuliza mama yake.

Juma: Eti mama ni kweli mchuma janga hula na wakwao?

Mama: Ndio mwanangu, ni lazima watakula pamoja

Juma: Kwani janga ni tunda hadi ale na ndugu zake?

Mama: Mwanangu huo ni msemo unaomaanisha kila baya unalolitafuta, utaathirika pamoja na ndugu zako, hivyo ni lazima kujiepusha.

**SWALI**

Taja matumizi tofauti ya chakula aina ya karanga

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mume afunga mwaka akidai talaka kwa fujo!

KARIBU MPENZI msomaji. Jamaa niliyemzungumzia wiki moja iliyopita kwamba "amejaribu kubomoa ndoa ya mwenzake akagonga mwamba", ndiye huyu huyu nitakayemzungumzia hapa, sasa maji yamemfika shingoni, amekuwa mbogo ametamka mbele ya wazazi kwamba anasubiri talaka toka kwa mkewe. Ikoje hii? Vuta pumzi nikumegee uone jinsi wenzio walivyoumaliza mwaka!

Jamaa huyu na mkewe walibahatika kuzaa mtoto mmoja wa kiume ambaye bado angali mdogo (miaka minne). Anamng'ang'ania mtoto ni balaa. Lakini swali, je, mtoto huyu bila mama yake atalelewa ipasavyo? Utakumbuka tulijadili karibuni kuhusu watoto wanaolelewa na mama walezi/kambo hujikuta wakiteseka, wengine kuwa mashoga.

Kinababa wengi hawana muda wa kufuatilia watoto kama ilivyo kwa mama. Ndio maana mtoto akibaki na baba yake asilimia kubwa wanaharibika ikiwa ni pamoja na kugeuzwa manunda (watukutu).

Hebu sikia mwendelezo kisa kilichopita, kisha utoe maoni au ushauri nini kifanyike;

Baada ya jamaa kushindwa kuvunja ndoa ya mwanaume mwenzake kule Moshi, sasa yuko tayari mkewe ampatie yeye talaka kila mtu asepe kivyake.

Mama baada ya kumuuliza mume wa mwanawe kwa nini apige simu na kuzungumza machafu juu ya binti yake ambayo yote alikana kuwa hayakuwa kweli, aliondoka zake kurejea Moshi. Kule alimweleza baba watoto wake kuhusu yaliyowasibu kule Dar ambayo alisababisha mume wa binti yao.

Baada ya majadiliano ya kina, baba aliamua kufunga safari kujua kwa nini kijana aendeleza mitafaruku dhidi ya mkewe kila kukicha kwa miaka mitano ya ndoa halali kanisani.

Baba kufika kikaitishwa kikao wakiwamo wazazi wa pande zote na viongozi wa dini. Baba wa binti alilazimika kuja Dar, kwa taarifa za bintiye kupigwa usiku kucha na kisha kuamriwa na mumewe kufungasha na kuondoka.

Binti aliripoti polisi kutokana na majeraha na kumfungulia mumewe RB. Kikao hicho kilijumuisha pia wanandoa hao wanaozozana kila uchao.

Binti alitoa maelezo, kisha mumewe kuzungumza na kuulizwa maswali. Yapo alijibu mengine alikaa kimya. Kwa mfano, kwa nini alimchania mkewe nguo za ndani na kuapa atazishughulikia na iko siku atarudi mwenyewe kwa kupiga magoti.

Kuhusu mtoto ambaye kwa wakati huo alikuwa ampeleka kwa mama yake (bibi mzaa baba), kwamba itakuwaje, jamaa alipaza sauti na kusema "mtoto wake asiguswe, atabaki naye na kwamba atampeleka akaishi na mama yake mzazi.

Mamake kusikia vile akaingilia kati na kusema hata yeye hamtaki mjukuu huyo kwa sababu ni mtundu sana hataweza kuishi naye, akitaka (babake) akae naye, hataki presha.

Kikao kilikuwa moto huku wanandoa wakitamka kila mmoja kumchoka mwenzake. Bibie akasema kama alidiriki kumfukuza nyumbani tena usiku wa manane kwa kumtolea nguo zake nje, katu hawezi kurudi acha ndoa ivunjike.

Binti akasema tayari ameshamfungulia mumewe RB polisi na kueleza vituko vyote na manyanyaso aliyowahi kufanyiwa na mumewe.

Kikao kile, hakikufikia muafaka unaoleweka. Wakati bado baba wa binti akitafakari yaliyojitokeza kikaoni, siku inayofuata mume wa bintiye alimpigia simu na kumweleza yafuatayo;

"Nimepigiwa simu na polisi nikihitajika kituoni kutoa maelezo baada ya mke wangu kutoa taarifa ya kupigwa... nimewajibu niko safarini ingawa niliwadanganya kwani nimejaa tele Dar.

Anasema haendi polisi na "ikitumika nguvu kunitafuta na kunikamata, kitakachofuata andaeni masikio yenu kuwasha...hamtakaa msahau".

Hilo ni tishio halipaswi kupuuzwa. Taarifa zingine zinasema kuwa mume huyo anasema anasubiri talaka ya mkewe yaani aachwe. Maneno haya yalimchoma sana baba wa binti kiasi cha kuamua kuwatafuta watu zaidi wanaomfahamu kijana huyo ili kujua tabia zake halisi.

Kabla ya kurejea Moshi, baba wa binti aliwatafuta viongozi wa kanisa ambao walimweleza fika tabia ya kijana kwani aliwahi kumshtaki mmoja wao kumdhulumu kiwanja ambacho kijana alipewa na askofu afanyie hapo biashara lakini yeye akataka kukitaifisha.

Ni muhimu kuchunguza marafiki muwajue kabla ya kuambatana nao, wengine ni mapepo. Hata maandiko ya Mungu yanasisitiza "uwe mwangalifu katika kuchagua marafiki".

**Hivi sasa wanandoa hao kila mmoja anaishi kivyake baada ya binti kuamua kwenda kukaa kwa baba yake mdogo baada ya kufukuzwa. Ama kweli Maisha Ndivyo Yalivyo. Je, una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Harusi ya Champagne, talaka ya bia na pombe za kupima

VISA vya wanandoa kutengana kwa shari, sasa ni kama utamaduni wa kawaida au fasheni.

Ukitazama kwa makini, utaona wanaoathirika zaidi kutokana na visa hivi ni watoto.

Wazazi hawapimi madhara ya kutengana kwao baada ya kupata watoto. Ni heri mtengane mkiwa hamjapata watoto au mtoto.

Fikiria huko Makambako, mkoa wa Njombe, tunaambiwa kuna kata, wanandoa 61 wamepeleka maombi ya talaka kwa ajili kuvunja ndoa zao katika Baraza la Kata.

Hiyo idadi ya wanaovunja ndoa ni waliojitokeza hadharani kwa kipindi cha mwezi mmoja na wiki mbili, kuanzia Novemba hadi Desemba 20, mwaka huu.

Kila anayekwenda kufungua shauri la kuvunja ndoa ili kupata talaka, inaarifiwa kwamba hakuna anayekwenda kwenye Baraza la Kata akasema anataka kusuluhisha, bali kila mmoja anasema sitaki tena ndoa.

Hivi huwa unajiulizaga kwamba ni kwa nini ndoa nyingi siku hizi hasa zile za Kikristo, wanapoingia ukumbini kusherehekea huanza na champagne?

Wakati champagne inafunguliwa mashuhuda huendelea kuwatizama huku wakigonga mvinyo wa bia, pombe kali.?

Katika hali ya kawaida kabisa, maharusi katika siku yao ya kwanza kuwa pamoja wanakuwa wamelewa! Wengine hulewa sana kiasi cha kusahau hata wajibu wao wa ndoa angalau kwa siku hiyo muhimu.

Licha ya Tanzania kuwa na Sheria ya Vileo na Sheria zingine ambatani, matumizi holela ya pombe zenye asilimia kubwa ya kilevi, yamekithiri mitaani na kusababisha madhara makubwa kwa jamii.

Ukienda baa, kwenye hizi glosari zilizoko mitaani, utakuta walio wengi hadi nyakati za usiku ni vijana, wanaume wenye umri wa kati kuanzia miaka 27 hadi 55 wanakunywa kupindukia. Nyumbani hakukaliki.

Wanapooana wanakunywa Champaigne iwe ya kilevi au haina kilevi, kwamba wanaruhusu kuongozwa na mvinyo.

Lakini mzozo wa ndoa au uhusiano unapochomoza, huyu anahamia kwenye bia, yule kwenye pombe kali, tena zile za kupima. Utaponea wapi zaidi ya kudai talaka na huyu kutoa talaka?

'Single mother' nao wamehamia baa, wanakunywa kupindukia, wanasema waziwazi kwamba bora kuwa 'single', unainjoi.

Ninayo kumbukumbu nzuri ya mwaka 2017, wakati serikali ilipopiga marufuku matumizi ya pombe zenye vifungashio vya plastiki maarufu kama viroba, baada ya kubaini kukithiri kwa tabia za ulevi na uchafuzi wa mazingira.

Hivi unajua wajanja hasa wafanyabiashara wa pombe, sasa wamegeukia kwenye chupa ndogo za plastiki mithili ya chupa za vitakasa mikono (sanitizer) zinazouzwa kwa bei nafuu ya Sh. 2,000.

Pombe hizo zina vilevi kati ya asilimia 35 hadi 43 na zinapatikana kirahisi kwenye maduka ya mitaani, vibanda vya wamachinga na hata kwenye vituo vya daladala.

Acha hizo pombe za kupima, kuna bia mbadala zenye ujazo wa mililita 350 zenye kilevi cha asilimia 4.5 hadi asilimia 5 zinazouzwa kati ya Sh. 1,500 hadi Sh. 2,500.

Kwa nini nimegusia vilevi kwenye hili la kuongezeka kwa wanandoa kutengana, talaka? Ni kwa sababu pombe ni moja ya vyanzo vya matatizo makubwa sana katika ndoa nyingi, ingawa wanandoa wanaokunywa huwa hawapendi sana kuzungumzia tatizo hili sugu.

Tatizo hilo ni kubwa sana, ingawa kwa Wamarekani nusu ya wanandoa wa Marekani ni walevi. Hii haijalishi kama mlevi ni bwana au bibi harusi wa ndoa hiyo.

Pombe imekuwa na madhara makubwa sana kwenye mahusianao ya wanandoa wengi kiasi cha kuathiri ndoa hizo. Baadhi ya madhara hayo ni:

Vurugu katika ndoa ni mambo yanayotarajiwa katika familia ya wanandoa walevi. Ugomvi wa mara kwa mara ni mambo ambayo yameripotiwa kwenye ndoa nyingi sana kote duniani.

Pombe inasababisha kuvunjika kwa mawasiliano miongoni mwa wanandoa. Mawasiliano kwa wanandoa ni moja ya matatizo makubwa sana kwenye ndoa. Makala maalum kuhusu mawasiliano italetwa kwenu siku zijazo.

Hasira ni moja ya matatizo yanayoletwa na pombe kwenye ndoa. Mwanandoa ambaye tabia yake ni ya kawaida, lakini baadhi wakinywa pombe wanabadilika na kuwa hasira nyingi na hilo linakuwa ni tatizo katika mahusiano yao Ulevi na pombe vinaweza kusababisha kutowajibika katika ndoa. Pombe inaweza kuwa inakula bajeti yote ya matumizi ya nyumbani kiasi cha kukosa kabisa fedha za kutunza familia.

Ulevi husababisha matatizo ya kisaikolojia kwa mwanandoa asiyekunywa. Matatizo hayo ya kisaikolojia yakichanganyika na matatizo ya huyo mwenzake mlevi basi ndoa hiyo itawaka moto.

Pombe ni chanzo kikubwa sana cha taraka na kuvunjika kwa ndoa. Mkusanyiko wa matatizo yote yaliyotajwa hapo juu yanachochea sana kuvunjika kwa ndoa.

Ulevi humfanya mwanandoa kujihusisha sana na wapenzi wengi sana.

Katika baadhi ya ndoa, matatizo ya ulevi yamehusishwa na mmoja kunyimwa unyumba.

Fakiria baba mlevi, mama mlevi, wote wanalewa kila siku wanarudi hoi na kwa wakati huo tendo la ndoa haliwezekaniki.

**Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 715 545 490**












Desemba 26, ilikuwa siku ya shangwe na nderemo kwa ndugu na jamaa wa maharusi Jackson Charles na Elizabeth Tesha, baada ya kufunga ndoa takatifu katika kanisa la Wasabato Kimanga, na kufuatiwa na tafrija fupi iliyofanyika katika ukumbi wa Hangaya, Segerea Dar es Salaam.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# FURAHIA 'SIXPACK' ukivaa mavazi haya...

HAKUNA kitu kinachowapagawisha wanawake kama kuwa na wanaume wenye umbo lililojengeka vyema na mikato imara ya tumbo maarufu kama Sixpack.

Hata hivyo, kutokana na desturi za kiafrika wanaume wenye miili ya aina hiyo wanakuwa hawana uhuru kwa kuogopa kuonekana miili yao.

Ni wazi wengi hawajui kwamba kuna aina ya mavazi wakivaa, hata wakionekana mikato ya miili yao hakuna tatizo lolote na badala yake inaonekana kama sehemu ya mitindo.

Kama wakitaka kuwa na furaha na wapenzi wao na wakati huo huo kudumisha desturi za Kiafrika zilizowakuza, basi angalia aina hizi za mavazi zitakusaidia.

**SHATI LA KUBANA**

Mtindo wa kuvaa shati la kubana na kisha kufunga vifungo viwili unafanya eneo kubwa la kifua na tumbo kuonekana vizuri. Hakikisha suruali inakuwa ya kubana pia ili kukupa mwonekano wa kupendeza zaidi.

**FULANA LAINI**

Vazi la fulana laini yenye kubana mwili pia linashauriwa kutumika endapo unataka kuonyesha mwili wako uliojengeka.

Jambo la kuzingatia hapa ni kuchagua fulana yenye kitambaa kinachoganda mwilini ili kukupatia mwonekano wa kuvutia.

**NGUO ZA UFUKWENI**

Nguo za ufukweni zinaonyesgha asilimia kubwa ya mwili na hivyo mikato ya tumbo na kifua huonekana kwa uwazi zaidi.

Hata hivyo, aina hii ya mavazi hutumika tu maeneo ya ufukweni wakati unapokwenda mapumziko, si vyema kuyavaa nyumbani au katika matembezi ya kawaida.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# NGOZI YA MTOTO

## Mtoto mchanga anatunzwa hivi......



MTOTO mchanga ni kiumbe dhaifu inatakiwa umakini wa hali ya juu kuhakikisha analindwa.

Mara anapozaliwa siku ya kwanza ulinzi unaotakiwa ni kumlinda na maambukizi yanayofanya ngozi kukauka.

Kwa hiyo, mzazi hapaswi kukimbilia kumuogesha mtoto mchanga, hasa anapokuwa katika mazingira ya hospitali.

Mkunga katika wodi ya uzazi ataeleza huduma gani utampa mtoto wako mchanga na jinsi ya kumuogesha unapofika nyumbani.

Vipodozi kwa ajili ya mtoto usikurupuke kumpatia ili kuepuka ngozi kukauka na kuharibika.

Mpake mafuta laini ya asili, epuka kumuongezea kwa mizaituni na krimu kwa sababu ngozi lazima inatakiwa kupumua wakati wote.

Unaweza kumuosha mtoto wako kila siku kwa maji safi na salama. Ni vyema kuepuka sabuni na vinywaji vyenye manukato.

Baada ya kumuogesha, kausha taratibu ngozi ya mtoto na ikiwa ni lazima maana unaweza ukaiacha ikauke yenyewe au kutumia kitambaa laini badala ya taulo.

Ukimaliza mpake cream ya maziwa au mafuta ya nazi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Andaa biriani la sikukuu



BIRIANI ni aina ya chakula pendwa hasa wakati wa sikukuu. Chakula hiki huliwa katika mchanganyiko wa mchele nyama ya ng'ombe, mbuzi, kuku au samaki.

Mahitaji

Mchele nusu kilo, nyama nusu kilo, vitunguu viwili, kitunguu swaum kijiko kimoja cha chai, tangawizi kijiko cha chai, maziwa mgando kikombe kimoja cha chai, hiliki nzima na mdalasini.

Mahitaji mengine ni karafuu nzima punje sita, pilipili mtama nzima punje 8, Curry powder nusu kijiko cha chai, binzari manjano nusu kijiko cha chai, binzari nyembamba nzima robo kijiko, chumvi na mafuta.

**Matayarisho**

Kaanga vitunguu hadi viwe brown, tia nyama na uikaange kwa muda wa dakika 10, baada ya hapo tia tangawizi, kitunguu swaum, hiliki, mdalasini, karafuu 4, pilipili mtama 5, Curry powder, binzari manjano, binzari nyembamba na chumvi.

Kisha koroga. Baada ya hapo tia maziwa mgando na uipike mpaka ikauke kisha tia maji kidogo, funika na upunguze moto uache ichemke kwa muda wa nusu saa. Baada ya hapo nyama itakuwa imeiva na mchuzi kubakia kidogo. Kwahiyo utatakiwa kuiipua.

Loweka mchele kwa dakika 10, kisha chemsha maji mengi kidogo katika sufuria kubwa. Baada ya hapo tia hiliki, mdalasini, karafuu, pilipili mtama, chumvi na mafuta kiasi.


Acha ichemke kidogo kisha tia mchele. Hakikisha maji yamejaa na uache uchemke kwa muda wa dakika 8 tu, halafu uipue na uchuje maji yote katika chujio.

Baada ya hapo chukua sufuria ya kuokea weka wali nusu na uusambaze sawia, weka mchuzi nyama na mchuzi wake pia utandaze na umalizie kwa kuweka leya ya wali uliobakia.

Ukimaliza ufunike na uweke kwenye oveni au kwenye moto wenye nyuzijoto 200 kwa muda wa nusu saa na baada ya hapo biriani litakuwa tayari kwa kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# WEKEZA KWENYE NYUMBA UPATE FAIDA

UJENZI wa nyumba ni miongoni mwa mambo muhimu yanayotumiwa na watu wengi kuwekeza.

Uwekezaji ni mchakato mzima wa kuiweka mali katika mfumo maalumu wa kifedha kwa ajili ya tija zaidi ya baadaye ambayo inaweza kuongezeka au namna fulani yenye kuleta faida baada ya muda fulani.

Leonald Michal, mshauri wa masuala ya uwekezaji, anaelezea kanuni bora za kuwekeza kwa tija. Anashauri kwamba unapowekeza kwenye ujenzi wa nyumba miongoni wa mambo ya kuzingatia ni pamoja na unataka kujenga nini kulingana na mahitaji katika uhalisia wa sasa na wa baadae.

"Kutazama ni aina gani ya watu watakaotumia nyumba yako, shughuli gani ambazo zitakuwa zinafanyika katika nyumba husika."

"Kwa hiyo ni muhimu pia kushirikiana na mtaalamu aliyebobea katika usanifu. Pia kujenga kwa kuzidi uwezo wako huleta hasara ya kushindwa kumaliza ujenzi, sehemu nyingine kutotumika na kutokuwa na faida ya kutosha, kutumia pesa nyingi kwa kitu kisicho na faida na kuwa na gharama kubwa za uendeshaji wa jingo," anasema.


"Pia kujenga kwa kutokidhi mahitaji, huleta hasara kwa kulazimika kufanya upanuzi wenye gharama kubwa zaidi, kuacha nyumba na kutafuta nyingine, kutoridhika na kutokuwa huru zaidi.Ni muhimu kuhakikisha kwamba unachojenga kitaleta faida kwa kipindi hicho cha uwekezaji," anaongeza.

Anashauri kwamba ni vyema kujiuliza maswali kama je, kodi ambayo wapangaji wanailipa inaleta faida? Mtaji uliotumia kujengea utakuja kujilipa baada ya muda gani? Faida ya kipesa itaanza kupatikana baada ya muda gani? Na je, nyumba yako itadumu kwa miaka mingapi?

Jambo lingine muhimu anasema unapowekeza katika nyumba ni kufuata sheria na taratibu zote husika ili uwekezaji wako usibughudhiwe na mambo mbalimbali ambayo yanaweza kuhatarisha mchakato wa kupata faida kwa kujenga katika eneo linaloruhusiwa kisheria na kwa kufuata sheria na taratibu zote.

Pia, anashauri kwamba makadilio ya gharama za ujenzi yatakusaidia namna ya kujipanga juu ya mtaji wa kukuwezesha kusogeza mbele na kwamba si vyema kujenga kwa kubahatisha.

Ni muhimu kuiona faida katika mipango yako ambayo umeifanya kabla ya kuanza ujenzi.



## Lifanye bafu kuwa la kifahari

**Na Restuta James**

UNAANZA na kumaliza siku yako bafuni. Ndiyo maana wataalamu wa mapambo wanashauri kwamba hiki ni chumba kinachopaswa kuwa na mazingira mazuri na ya kifahari.

Ili kukifanya chumba hiki kivutie, wanashauri uweke marumaru nusu ukuta ili iwe rahisi kubadilisha mwonekano pale unapohitaji kufanya hivyo.

Hata hivyo, kwa wale ambao wameweka marumaru ukuta mzima, siyo tatizo sana kwani kuna namna nzuri ya kupendezesha bafu na choo chako.

Wataalamu wanaeleza kuwa kwa ukuta wenye marumaru nusu, chagua rangi tatu lakini moja ipakwe eneo la asilimia 70, ya pili ipakwe asilimia 20 na nyingine asilimia 10.

"Sheria ya rangi tatu inakuwezesha kuunda ufahari ambao ni vigumu kukosa kuifurahia bafu yako," inasema sehemu ya taarifa ya wataalamu hao.

Wanaeleza kuwa mabafu na vyoo ni miongoni mwa vyumba vigumu kupamba kwa sababu ya vifaa vingi visivyohamishika kama makabati na masinki, lakini unaweza kubadili mwonekano wa eneo dogo kadiri inavyowezekana.



Kwa wanaotaka kubadili mwonekano wa rangi, kijani kisichokolea ni rangi maarufu ya bafuni mwaka huu kwa sababu inatoa mandhari ya kutuliza na kuburudisha akili.


Rangi hii inaweza kutawala kwa asilimia 70, chokaa ikawa kwa asilimia 20 na asilimia 10 ikawa ya mzeituni.

"Kwa mwonekano wa kifahari, unaweza kupaka chumba kizima rangi ya kijani kisichokolea," wanashauri.

Inaelezwa zaidi kwamba rangi ya bluu tulivu, imekuwa mashuhuri kwa ajili ya chooni kwa miongo kadhaa kutokana na uwezo wake wa kuleta utulivu na mvuto.

**Tuwasiliane kupitia 0753 33330, barua pepe restutajames@gmail.com**

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
kwa heri 2023 karibu 2024
SHEMELA TUNA-UAGA VIPI MWAKA 'HATUTOKI OUT?'
NIHAKIKISHIE TUKIWA BAR NIKIKUTONGOZA NI POMBE
JUKWAANI
!
'MAISHA'
SISI
HAKABWI MTU JIACHIENI MKESHA 'MWAKA MUPYA'
HIYO ZAWADI KUBA SANA NAKUPA VEVE UKAWEKEE TOTO YAKO IONE 'MAKA MPYA'
SIJAFIKA MBALI ISHANI-CHUBUA BEGA
INCHI'32 KILO 40
UJIO WA MWAKA MPYA WENZETU WANA-FAGILIA MOYO SISI TUNAKAANGA FIGO!
POMBE GANI KIKIJAA KISODA UMELEWA! KAMA SIO KUUANA
ULINIAMBIA MWAKA HUU LAZIMA UTOBOE HAYA NAMBIE
LABDA '2024' LAKINI 2023 NIME-AMBULIA KUTOBOA SIKIO!
UMEAMUA MWENYEWE KUNITOA MKESHA WA MWAKA MPYA, SASA SITAKI KUBANWABANWA NIACHE NIJIACHIE
UBANWE KWANI UNAENDA KUVALISHWA "SKINI TAITI"
*KINYUNYIZO CHA LEO...
'heri ya mwaka mupya wasomaji wote wa safu hii pendwa asanteni kwa sms zenu'

## HABARI KIMATAIFA



Mwanamke wa Kipalestina akipika chakula akiwa katika hema mjini Rafah baada ya kukimbilia eneo hilo kutokana na mashambulizi ya jeshi la Israel yanayoendelea Ukanda wa Gaza. PICHA: REUTERS

# Afrika Kusini yaishtaki Israel ICJ, yadai Gaza kuna mauaji ya halaiki

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

AFRIKA Kusini imefungua rasmi mashtaka katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ), dhidi ya Israel ikidai inahusika na vitendo vya mauaji ya halaiki katika Ukanda wa Gaza.

Mahakama hiyo iliyoundwa na Umoja wa Mataifa, ilithibitisha shauri hilo kufunguliwa na kujikita zaidi katika madai ya ukiukaji wa majukumu na kukiuka mkataba wa kimataifa unaozuia mauaji ya kimbari.

Hata hivyo, Israel ilikanusha vikali madai hayo na kuyataja kuwa hayana msingi.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje ilisema nchi hiyo inakataa madai hayo na kuchukizwa na kashfa inayoenezwa na Afrika Kusini.

Mahakama hiyo ya kimataifa ambayo makao makuu yake yako The Hague nchini Uholanzi, ndicho chombo kikuu cha sheria kinachotambuliwa na Umoja wa Mataifa.

Baadhi ya majukumu yake ni usuluhishaji wa migogoro kati ya mataifa wanachama na kutoa ushauri wa kisheria katika maswala mbalimbali ya kimataifa.

Baada ya kufungua mashtaka hayo, ofisi ya rais wa Afrika Kusini ilisema katika taarifa kwamba nchi hiyo inalazimika kuzuia mauaji ya kimbari kutokea ukanda wa Gaza.

"Afrika Kusini inasikitishwa na hali mbaya wanayokabiliana nayo raia walionaswa katika mashambulizi ya sasa ya Israel katika eneo la Ukanda wa Gaza, kutokana na matumizi ya nguvu ya kiholela na kuwahamisha watu kwenye makazi yao kwa nguvu," ilisema taarifa hiyo.

Iliongeza "kuna ripoti zinazoendelea za uhalifu wa kimataifa, kama vile uhalifu dhidi ya ubinadamu na uhalifu wa kivita unaofanywa pamoja na Israel. Vitendo hivyo vinakidhi kizingiti cha mauaji ya kimbari au uhalifu unaohusiana nao, vimefanywa na vinaweza kufanywa katika muktadha wa mauaji yanayoendelea Gaza."

Mshtaka hayo yenye kurasa 84 yalisema kuwa vitendo vinavyofanywa na Israel ni mauaji kamili ya halaiki kwa sababu vinakusudiwa kuleta uharibifu sehemu kubwa ya Taifa, kundi, rangi na kabila la Palestina.

Katika mashtaka hayo, nchi ya Afrika Kusini inaitaka mahakama hiyo kusikiliza kesi hiyo wiki ijayo na kwamba hatua za haraka zitolewe na mahakama hiyo, ikiwa ni pamoja na Israel kusitisha shughuli zote za kijeshi ndani ya Gaza.

Wakati huo huo, vikosi vya Israel vinaendelea kuvamia maeneo mbalimbali ya Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kimabavu.

Shirika la Habari la Palestina (WAFA) lilisema maeneo hayo ni pamoja na kambi ya wakimbizi ya Balata na miji ya Qasra na Beita, mashariki mwa Nablus. (Wafa).

Katika taarifa yake ilisema kijana mwingine mwenye umri wa miaka 16 kutoka kambi ya Al-Fawwar, kusini mwa Hebron, aliuawa kwa kupigwa risasi na wanajeshi wa Israel.

Katika tukio hilo, Wapalestina wanne walijeruhiwa wakati wa makabiliano na majeshi ya Israel yalipovamia mji wa Yatta, kusini mwa Hebron.

Jeshi la Israel (IDF) lilisema kikosi cha wanamaji wameshambulia eneo lote la Ukanda wa Gaza katika vita vikali inayoendelea.

Taarifa hiyo ilisema vikosi vingine vilivyokuwa mji wa Gaza viliwaua watu kadhaa waliowaita kuwa magaidi.

Wanajeshi hao pia walihar ibu majengo mawili yanayodaiwa kutumiwa na Hamas katika eneo la Beit Lahiya kaskazini mwa Gaza.

Wizara ya Afya inayosimamiwa na Hamas huko Gaza ilisema kuwa watu 187 waliuawa katika mgomo katika kipindi cha masaa 24.

Aidha, Ofisa mkuu wa afya wa Hamas, alisema Wapalestina 100 wameuawa na wengine 158 wamejeruhiwa katika mashambulizi yaliyofanywa na Israel kwa muda wa saa 24 zilizopita.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA), imekadiria kuwa watu 100,000 wamehamia mji wa Rafah katika siku chache.

Siku za hivi karibuni jeshi la Israel liliwataka watu kuondoka haraka maeneo ya Khan Younis, ambayo inachukulia kuwa ngome ya wanamgambo wa Hamas.

OCHA ilisema kufurika kwa watu katika eneo hilo kumesababisha msongamano kuwa mbaya zaidi.

Pia ilieleza kuna wasiwasi kuongezeka na kuenea kwa magonjwa ya milipuko.

**BBC**

# Mshindi urais DRC kujulikana leo

**KINSHASA,** DRC

MSHINDI wa uchaguzi mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), atajulikana leo baada ya Tume ya Uchaguzi nchini humo kumaliza kujumuisha kura na kutangaza matokeo ya mwisho.

Tangazo lililotolewa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi (CENI), Denis Kadima, lilisema tume hiyo itaheshimu muda kwa kukamilisha utoaji wa matokeo kama ilivyopanga kutoka katika vituo vyote vya kupigia kura nchini kote.

Hadi kufikia jana, CENI ilisema ilihesabu kura karibu milioni 16, huku matokeo yakionyesha kuwa Rais Felix Tshisekedi anaongoza kwa asilimia zaidi ya 77.

Uchaguzi huo uliofanyika Desemba 20, umekosolewa na wagombea wa upinzani walioandaa maandamano jijini Kinshasa, kushinikiza kufutwa kwa uchaguzi huo.

Kulingana na taratibu za kisheria, baada ya matokeo hayo kutangazwa, mahakama ya katiba inatakiwa kuyathibitisha mwezi Januari mwakani na mshindi ataapishwa Januari 20.

Waangalizi wa ndani kutoka mashirika ya kiraia na viongozi wa Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki (CENCO) wamekosoa uchaguzi huo na kuutaja kuwa na dosari nyingi.

Zoezi la upigaji kura lilifanyika kwa siku mbili baadhi ya maeneo baada ya vituo kuchelewa kufunguliwa, kuchelewa kupokelewa kwa vifaa vya kupigia kura na vituo vingine kutofunguliwa kabisa.

**RFI**

**Hadi kufikia jana, CENI ilisema ilihesabu kura karibu milioni 16, huku matokeo yakionyesha kuwa Rais Felix Tshisekedi anaongoza kwa asilimia zaidi ya 77.**

# Serikali Senegal yazuia mkutano wa upinzani

**DAKAR,** SENEGAL

SERIKALI ya Senegal imepiga marufuku mkutano wa kumuidhinisha kiongozi wa upinzani Ousmane Sonko kugombea nafasi ya urais katika uchaguzi wa urais utakaofanyika mwakani.

Gavana wa mji mkuu Dakar, Cherif Mouhamadou Blondin Ndiaye, alisema katika taarifa yake kuwa wameufuta mkutano huo kutokana na kuwepo viashiria tishio la nchi, kuvuruga shughuli za umma na kuwepo hatari ya watu wenye nia mbaya kujipenyeza kwenye mkusanyiko huo.

Sonko aliwasilisha nyaraka zake katika baraza la katiba ili kuwa mgombea wa urais katika uchaguzi utakaofanyika Februari, licha ya serikali kukataa kumpa nyaraka muhimu.

**DW**

## MAKALA

# SIASA NI MAISHA, USIJITENGE NAYO



Na Magabilo Masambu

"Every human being is a political animal" Ni maneno ya mwanafalsafa mkongwe wa Ugiriki, Aristotle, akiwa na maana kwamba kila mwanadamu ni mwanasiasa! Anasema siasa ni hali ya kufikia makubaliano kwa njia ya ushawishi na kujenga uhusiano. Yaani kama umewahi kufanya jambo lolote ukafikia makubaliano na mwingine basi wewe ni mwanasiasa.

Anajaribu kuwafananisha wanadamu na wanyama aina ya ndege kwa tabia yao ya kuruka na kupaza sauti mwituni haki wanayozaliwa nayo, hata siasa ni hivyo. Jiulize katika maisha yako yote hujawahi kumshawishi yeyote mkakubaliana? Kama umewahi na ukafanikiwa wewe ni mwanasiasa nguli. Wako baadhi ya watu wanasema wao si wanasiasa wakidhani kwamba siasa lazima uwe diwani, mbunge au Rais wa nchi jambo ambalo si kweli.

Kwa mujibu wa Ibara ya 8(a), (b), (c) na (d) ya katiba ya nchi yetu inaweka wazi kuwa wananchi ndiyo wenye nchi, uamuzi wowote utakaofanywa na wanasiasa lazima uzingatie misingi ya demokrasia, bahati mbaya tulio nayo Afrika ni kudhani kwamba demokrasia ni kuwa na vyama vingi vya siasa pekee. Lakini uamuzi wowote unaohusu maisha ya watu lazima uwe umepata nguvu ya ushawishi badala ya ushawishi wa nguvu. Hata ushiriki huo uliotajwa na katiba kipengele (d) lazima uwe umejengwa katika misingi hiyo.

Wajibu mkubwa wa wanasiasa si kuwaletea wananchi maendeleo na katika hili wanasiasa wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kuwafanya watu waamini kwamba maisha yao yatajengwa na wao na kwamba bila wao maendeleo hakuna, jambo ambalo si kweli kwa sababu hakuna mwanansiasa hata mmoja anayetumia fedha yake mfukoni kuleta maendeleo au fedha hizo zitakuwa zimetokana na rasilimali zetu za nchi, kodi au mikopo ambayo pia walipaji ni wananchi au misaada kutoka nje.

Kipengele (b) Ibara ya 8 kinasema lengo kuu la serikali litakuwa ustawi wa wananchi, ustawi wa jamii si katika eneo moja tu la maendeleo ya vitu kwa maana ya barabara nzuri, mwonekano mzuri wa miji na kadhalika. Ustawi huwo ni pamoja na uhuru wao, kuongozwa kwa mujibu wa katiba, kuwa na uhuru wa kusema hili sawa, hili hapana na wakisema hili hapana katiba ilinde uhuru huo na kazi ya wanasiasa iwe ni kutumia hoja nzuri za kuwashawishi wakubali kwa hiari yao baada ya kuelewa vyema juu ya jambo lenyewe.

Kwa maana nyingine wajibu wa wanasiasa ni kuwakilisha mawazo na maoni ya wananchi pamoja na kuwaunganisha, ndiyo maana tunavyo vyombo vya uwakilishi kama bunge na kwa sababu wananchi ndiyo waajiri kwa mujibu wa kifungu kidogo (a) cha ibara ya 8 maoni na malalamiko yao ni muhimu kusikilizwa ama kuyafuta malalamiko au kuwashawishi waone umuhimu wa kutekeleza jambo fulani wanaloona haliko sawa.

Nakubali kwamba si mambo yote yanayopaswa kutekelezwa na wanasiasa lazima yote yawe ni ya wananchi, yaweza kutoka kwa wanasiasa pia maana wao nao ni sehemu ya wananchi, kazi kubwa watakayokuwa nayo si kutumia nguvu kuyalazimisha mawazo yao, bali kujenga hoja juu ya mambo hayo.

Mtu yeyote atakayeshindwa kujenga hoja ya ushawishi badala yake akatumia nguvu kulazimisha jambo fulani lifanyike, lazima ajihesabu kwamba siasa imemshinda, hivyo achukue jembe akalime kwa kuwa akiendelea atasababisha matatizo makubwa.

Kuelekea mwaka 2024 katika nyanja ya maendeleo lazima tubadili fikra za kuamini kwamba sisi wananchi tunatakiwa kuletewa maendeleo na wanasiasa, bali wananasiasa wanapaswa kuweka mazingira wezeshi na usimamizi mzuri wa rasilimali zetu ili wananchi wajiletee maendeleo.

Kama tutakuwa na wanasiasa wanaoshindwa kusimamia rasilimali zetu ndani ya nchi, katiba imetupatia nafasi ya kuwaondoa katika nafasi zao kupitia sanduku la kura, kwasababu watakuwa wameshindwa kutenda wajibu wao kama wananasiasa.

Mwisho, siasa ni nyepesi sana kama zitatumika akili za kutosha badala ya nguvu ambazo zinaweza kufanikisha jambo kwa muda mfupi na kuleta madhara makubwa. Tanzania kwa nchi za Afrika kutokana na misingi tuliyokuwa nayo huko nyuma hasa umoja, amani na upendo, hatukuwa na nchi ya kufananishwa nayo wengi walikuwa wanafunzi wetu. Turudi kwenye misingi yetu ya utaifa inayojumuisha utamaduni, historia na mila zetu lakini muhimu zaidi kuenzi mambo mazuri ya wazee na vongozi wetu ambao baadhi wametangulia mbele ya haki.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Busu pande tatu za uso, penzi lajisuta lenyewe



Na Adam Fungamwango

UMESHAWAHI kusikia au kuona penzi linajisuta lenyewe? Nadhani umeshawahi kuona, kusikia au likakukuta, ila tu kujua kuwa hapa penzi limejisuta ndiyo mtihani.

Mara nyingi penzi linalojisuta ni lile ambalo halikuanza na misingi ya penzi la kweli.

Siku zote penzi la kweli hujidhihirisha nyakati zote za dhiki, faraja, raha na tabu.

Wapenzi watapitia hali ya shida na shaka lakini kwa sababu limewekwa kwenye misingi imara, yote yanapita na lenyewe linaendelea kusonga mbele.

Sasa kwenye penzi ambalo lipo kwa sababu zilizo nje ya hapo ndiyo tatizo.

Kwenye maisha yetu ndani ya jamii, kuna mapenzi ya kweli na ya uongo.

Kuna wanaojifanya wanawapenda wenzao kwa sababu ya pesa. Zinapoisha ndipo linaanza kujisuta. Yaani kila mtu sasa anajua kumbe haikuwa kweli. Penzi lilijivika ngozi ya kondoo wakati kumbe ni chui. Hiyo haswa huwa kwa upande wa baadhi ya wanawake. Pia kuna wanawake hujiingiza kwenye mapenzi na wanaume kwa sababu ya kutaka ndoa fupi.

Yaani na yeye aingie kwenye vitabu vya wanawake ambao wameshawahi kuolewa. Utamjuaje mwanamke wa aina hii?

Hata mwezi bado tangu muwe pamoja, lakini keshaingizia suala la kuolewa wakati wote wawili bado hamjafahamiana vizuri tabia zenu. Hawa wakishaingia kwenye ndoa, baada ya muda mfupi tu ndoa inaanza kujisuta.

Siku hizi ambapo kinadada wamekuwa na vikundi vya kutunzana, kupeana zawadi kwa zamu, kusaidiana, kuchangiana kila mmoja anapokuwa na jambo lake la kijamii kama msiba au sherehe, wamekuwa wakizitafuta ndoa kwa lazima ili na wao wachangiwe.

Wanapoona wenzao wanatunzwa friji, vitanda, makochi, feni, kabati, televisheni, deki na fanicha mbalimbali na wao wanaanza kulazimisha kuingia kwenye mapenzi kwa mtu ambaye anaona anaweza kumuoa, lakini moyoni mwake hampendi.

Yuko anayempenda kwa dhati lakini hana uwezo huo. Kwa hiyo hukimbia kwa mtu ambaye angalau anaweza kufanya hivyo. Nia hapo si mapenzi wala ndoa bali na yeye achangiwe na wenzake kama yeye anavyochanga kila mara. Inakuwaje yeye achange halafu yeye asichangiwe?

Anapopata hivyo vitu ndipo uongo na ukweli unaanza kujitenga. Hakuna mapenzi ya kweli kwa mwanaume. Alichotaka ameshakipata. Penzi na ndoa vinaanza kujisuta. Na wanawake wa aina hiyo anaweza kuachika, halafu akataka kwenda kuolewa na mtu mwingine kwa sababu hiyo hiyo.

Hata wanaume nao wako baadhi wana tabia kama hii. Hupenda kuwaongopea kinadada au kinamama kuwa watawaoa. Uchunguzi wangu mdogo kwanza kabisa nimebaini, wanawake wengi wanapenda kuolewa.

Wanawake wengi unapowaambia kuwa nitakuoa au nataka nikuoe, hata kama alikuwa hakutaki, anaweza akaweka silaha chini.

Na hii ndiyo sababu baadhi ya wanaume ambao hawana kipaji cha sanaa ya kuwashawishi wanawake wenye misimamo kuingia kwenye uhusiano huamua kutumia silaha hii.

Uchunguzi wangu wa pili umebaini kuwa baadhi ya wanaume kwa sababu ya 'domo zege', wamekuwa wakitumia kauli kuwa nataka nikuoe, lakini lengo si hilo bali ni kumpata tu ili aendelee na hamsini zake.

Anapofanikiwa, ndipo mwanamke anapoanza kuona rangi halisi ya mpenzi wake hapo ndipo penzi linaanza kujisuta.

Mwanzoni penzi moto moto, mabusu kama yote usoni, lakini mwisho wa siku linatoweka hata majivu hayaonekani.

Na hili wamelithibitisha wanamuziki wa bendi ya Bima Lee Orchestra, mwishoni mwa miaka ya 1980, walipofyatua kibao walichokiita 'Busu Pande Tatu', ambacho kilitungwa na Maximillian Bushoke, akiimba kwa hisia kali na Jerry Nashon 'Dudumizi' (sasa marehemu). Hapa ndipo utajua penzi linavyojusuta.

"Vipi mbona sasa wajisuta mwenyewe, ulipokubali kunipenda hukulazimishwa.

Uliahidi kwa ahadi na viapo pia, uliahidi kwa ahadi na viapo pia, mwanzoni lilikuwa penzi moto moto, mwanzoni lilikuwa penzi moto moto, busu pande zote tatu za uso ooo.

Kila mara ahadi za kuonana zilikuwa haziishi, ulikuwa haushi kuniuliza, darling wapi leo tukatumie, darling leo wapi tukale kuku, darling wapi leo tukatumie.

Kumbe ulikuwa na lako moyoni, ulipolipata ukabadilika, sasa nimebaini.

Ukweli nimeuona kwenye hili penzi letu, mwenye pendo la udanganyifu sasa ameonekana, ukweli nimeuona kwenye hili penzi letu, mwenye pendo la udanganyifu sasa ameonekana.

Kwenye mapenzi ya kweli watu huvumiliana, kwenye dhiki na faraja, wote hushirikiana, kwenye mapenzi ya kweli watu huvumiliana, kwenye dhiki na faraja, wote hushirikiana.

Kiko wapi sasa jama eee, maneno uliyonieleza, nakupenda hakuna mwingine tena, kumbe yote ni uongo, kiko wapi sasa jama eee, maneno uliyonieleza, nakupenda hakuna mwingine tena, kumbe yote ni uongo.

Ama ni kweli mapenzi hayana mdhamini nimeamini, yaweza vunjika wakati wowote, ama ni kweli mapenzi hayana mdhamini nimeamini, yaweza kuvuka wakati wowote.

Uko wapi sasa moto wa mapenzi yetu mimi na we? Uko wapi sasa moto wa mapenzi yetu mimi na wewe? Mbona umezimika hata majivu hayaonekani, mami, mamiii!

Ama ni kweli mapenzi hayana mdhamini nimeamini, yaweza vunjika wakati wowote.

Ama ni kweli mapenzi hayana mdhamini nimeamini, duniani, duniani siku hizi, ama ni kweli mapenzi hayana mdhamini nimeamini, duniani, duniani siku hizi.

Ilove you, busu nyingi, uongo, uongo, bibiii, sheri iii, sheri iii!"

Aisee, ni hatari tupu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi.
Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa.
Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.
Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Kassim aliona aibu kidogo, kwani alikumbuka aliambiwa atoe pesa kidogo, lakini akapotezea.

Leo bila kutoa pesa analetewa chakula.

Sauda alitoa hotipoti kwenye kikapu chake, akaweka mezani. Alichofanya Kassim na kwenda kununua soda ili wakila washushie.

Kitendo cha Sauda kutaka kula na aliyemletea kikaondoa dhana ya Kassim ya kuwekewa limbwata.

"Ingekuwa hivyo yeye asingekula." akajiambia.

Wakala kwa pamoja. Utamu wa chakula ulimshangaza Kassim

"Umepika wewe hiki chakula?"

"Nani mwingine?"

"He, kama ni hivyo wewe kumbe ni mkali mpaka kwenye jiko!"

"Nashukuru Mungu kwa hilo mpenzi."

Tangu siku hiyo, Kassim akawa anatoa pesa ya kula kwa Sauda ili awe anamletea chakula usiku.

Na si hivyo tu, hata kama siku dada yake Sauda akikwama, Kassim anachukua nafasi ya kurekebisha mambo watu wale.

Ndipo alipoamini kuwa Sauda ni mwanamke ambaye pia anajua mapishi hasa. Hakurudia tena kula mgahawani.

Kuna siku Sauda aliomba apewe pesa shilingi elfu hamsini. Kwa haraka haraka ilikuwa ngumu kwa Kassim, lakini kwa sababu tayari alishakuwa na uhusiano na kimapenzi naye aliona si vibaya kumpa wake akipendacho.

"Sawa ila siyo leo."

"Na mimi sikusema unipe leo, utakapopata." Akajibu Sauda.

Alipopata alimkabidhi Sauda ili akamalizie matatizo yake yanayomkabili ambayo Kassim hakutaka kuyauliza.

Siku mbili baadaye aliporejea nyumbani kwake alikuta pazia mpya ya mlangoni na za madirishani. Shuka moja mpya na foronya mbili za mito.

Ndipo Kassim alipogundua kuwa kumbe zile pesa alizoomba haikuwa kwa ajili ya matatizo yake.

Ilikuwa ni kubadilisha mazingira yaliyokuwemo ndani. Na kweli, tangu aondoke Siwatu hakubadilisha chochote ndani.

Pazia na foronya zilizokuwepo zilikuwa moja kati ya vitu vichache vilivyoachwa na Siwatu aliyesomba zaidi ya asilimia 90 ya vitu vyote ndani mle.

"Huyu mwanamke huyu!" Akashangaa Kassim kimoyomoyo.

"Kumbe zile pesa alizokuwa anaomba siyo kwa ajili ya matatizo yake, ila ni yangu."




**"Nina nia nzuri tu na mdogo wako, kusema kweli nimempenda kwa mambo mengi, ikiwemo hata akili na tabia yake nzuri, nimefanya hivi kwa sababu akikaa sana hapa inawezekana kuna mtu anaweza kuja jumla hapa, au huko Kondoa ikapelekwa barua nimamkosa Sauda wangu," akalalamika Kassim. Ni kweli kabisa, kwake Sauda kwa sasa alikuwa kila kitu.**

Kwa macho yake kwa sababu yamezoea, aliona kawaida tu, lakini kumbe tayari kwa mapazia yameshapauka na yamekuwa makukuu.

Jicho jipya la Sauda liliona pazia za mlango zimeshachakaa. Hakutaka kumwambia mwenyewe. Ni mwanamke aliyefundwa akafundika. Atamwambia kwa vitendo siyo maneno.

Unawezaje kumwambia mwanaume unayempenda, "mbona pazia za mlangoni na madirishani zinakauka? Mbona shuka na foronya zimachakaa?"

Alichofanya ndiyo hicho alichofanya, kitu ambacho kilizidi kumkonga nyoyo Kassim.

"Huyu ndiye mwanaume niliyekuwa wanamsubiria siku zote. Huyu ndiye yule ambaye mama yangu angetaka kumuona siku ya harusi tangu." Akawaza.

Tangu hapo, Kassim akakubali kuwa Sauda ndiye mwanamke wa maisha yake na alichelewa sana kumpata.

Ndani kulibadilika. Sauda alianza kubadilisha kila kitu. Alinunua vitu vingine vya kuipendezesha nyumba na hata mtu akiingia tu moja kwa moja hajiulizi mara mbili kama anaishi mwanamke mle ndani.

Kumbe huwa anakuja jioni, usiku, na kuondoka asubuhi wakati akiwa ameshafanya usafi kurudi kwa dada yake.

Kassim akanogewa. Alichofanya ni kwenda kwa dada yake na kumuomba rasmi Sauda akae kwake.

Hakupinga, ila akasisitiza asimharibie maisha mdogo wake, kwani akisema wanaume wengi wana matatizo.

"Unaweza kumchukua mdogo wangu hapa kwa raha na bashasha, ukampa ujauzito unamruka futi mia moja. Mimi sina tatizo, ila unamchukua hapa, kwetu Kondoa, kuna wazazi kule, unatakiwa uende kujitambulisha." Ulikuwa ni ushauri wa dada yake Sauda.

"Nina nia nzuri tu na mdogo wako, kusema kweli nimempenda kwa mambo mengi, ikiwemo hata akili na tabia yake nzuri, nimefanya hivi kwa sababu akikaa sana hapa inawezekana kuna mtu anaweza kuja jumla hapa, au huko Kondoa ikapelekwa barua nimamkosa Sauda wangu," akalalamika Kassim. Ni kweli kabisa, kwake Sauda kwa sasa alikuwa kila kitu.

Mwanamke aliyemrudisha tena kuwa binadamu. Aliyemfanya kujua duniani kuna kupenda na kupendwa. Aliyemfanya aanze kukaa nyumbani kwa muda mrefu zaudi kuliko baa. Mwanamke aliyemfanya akili yake ianze kufahamu kuwa siyo kila mwanamke ni mbaya kama alivyokuwa anadhani baada ya matendo aliyofanyiwa na mchumba wake wa mwanzo, Siwatu.

Rasmi Sauda akahamia nyumbani kwa Kassim, pika na kupakua. Baada ya mwaka mmoja kupita ilikuja taarifa kuwa baba yake Sauda ni mgonjwa huko Kondoa, hivyo inabidi aende kumuana.

Halikuwa jambo gumu kwa Kassim, alimkatia tiketi, akamfungashia na vijizawadi vya mama, pesa ya akiba kwa lolote litakalotokea kama akichelewa, na akamsindikika mwenyewe hadi kwenye Kituo cha Mabasi ya Magufuli.

Wiki mbili zilipita. Kukaa peke yake kulimchosha Kassim. Tayari adha hiyo alishaondokana nayo. Alishazoea kukaa na mpenzi wake Sauda.

Mwezi mmoja alivyotimia, akaambiwa na mchumba wake Sauda kuwa hawezi kurudi tena huko.

"Wamenizuia." Aliongea kwa sauti dhaifu kwenye simu.

"Nani kakuzuia?"

"Baba."

"Kwa nini?"

"Kasema mpaka wewe uje huku."

"Kwani kuna nini Sauda? Mbona hutaki kuniweka wazi?"

"Dada keshawaambia huku kuwa ni mwanaume. Na nakaa naye. Kwa hiyo hata huu ugonjwa wa baba haukuwa wa kweli. Nilivyokuja huku nimesemwa kweli. Nikaambia nakaa na mwanaume muda wote bila kumpeleka kujitambulisha nyumbani."

"Kwa hiyo wanatakaje?"

"Wewe uje ujitambulishe kwao, wakufahamu, mengine watakuja kukwambia wao wenyewe."

Yalikuwa ni mazungumzo ya simu kati ya Kassim na mpenzi wake Sauda.

Ingakuwa ni yale tu mapenzi ya mwanzo, Kassim wala asingejisumbua kwenda. Kwa sasa Sauda alikuwa amejaa moyoni mwake.

Hakuweza kufanya chochote bila Sauda. Kwake alikuwa ndiyo kila kitu.

"Hakuna yoyote aliyeleta barua huko?" N swali alilouliza kesho yake.

"Sijui, lakini sidhani, ningekuwa nimeshaambiwa. Ila ndugu yangu kama unanihitaji ufanye haraka uje."

"Wala haina tatizo, waambie mwanzoni mwa mwezi nakuja. Hasubiria mashahara wangu mwisho wa mwezi."

"Nakushauri uje na mtu. Huyo mtu ndiyo awe kama mshenga. Uwe na barua kabisa. Unajua angalau ukitoa barua tunaweza hata tukajenga hoja wakaniachia." Sauda akashauri.

"Ni kweli mpenzi wangu, umetoa wazo wa busara sana. Na ndicho ninachokupendea mpenzi wangu." Akajibu.

"Ahsante sana mpenzi, nakutegemea utakuja, hutoniangusha."

Itaendelea Jumapili

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# TIWA SAVAGE KULIKONI TENA?

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Nigeria, Tiwa Savage, amezidi kuwasha moto kwa mashabiki zake baada ya kusisitiza ana mapenzi makubwa na msanii mwenzake Flavour.

Kupitia Instagram, hivi karibuni Savage alifichua kuwa anavutiwa na Flavour kutokana na kipaji chake baada ya kuulizwa na mashabiki zake kama atapanda jukwaani katika jiji la Logos siku zijazo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 43, amesema mwimbaji huyo mwenye mwili uliojengeka anapenda kutazama maonyesho yake na ataendelea kufanya hivyo.

# ADDICTED YAZIDI KUMPAISHA TARISAI VUSHE

Mwimbaji wa gospo kutoka pande za Australia, Tarisai Vushe, amewashukuru mashabiki wa muziki wake kwa mapokezi mazuri ya video ya wimbo wake unaoitwa Addicted iliyotoka mapema mwezi huu.

Tarisai mwenye asili ya Zimbabwe, amefanikiwa kuwababamba mashabiki wa muziki nchini kwa aina ya uimbaji wake.

“Nimeona mapokezi ya Addicted ni makubwa, namshukuru Mungu vijana wengi wa nyumbani Afrika wameipokea vizuri huu ni mwanzo wangu mzuri wa kutoa wimbo mwingine mwezi Februari,” amesema Tarisai.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**MADRID YAMFUATA MBAPPE**
REAL Madrid watafanya jaribio jipya la kumnunua mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 25 na wamempa hadi katikati ya Januari kuamua iwapo anataka kujiunga nao majira ya joto. **(-Athletic)**

**MBAPPE ATAJWA LIVERPOOL**
LIVERPOOL iko mbioni kumsajili, Kylian Mbappe, kwa sababu ana uhusiano mzuri na klabu na kocha, Jurgen Klopp. **(Talksport)**

**OSIMHEN ANUKIA ARSENAL**
ARSENAL inamtaka mshambuliaji wa Napoli mwenye umri wa miaka 25, Victor Osimhen, mshambuliaji wa Bayer Leverkusen na Nigeria, Victor Boniface (23) na mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez (26), kama mbadala wa mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney (27). **(Express)**

**PHILLIPS NJIA MOJA**
KLABU ya Manchester City imeanza mazungumzo na Juventus kuhusu kumwachia kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, mwenye umri wa miaka 28 kuondoka kwa mkopo. **(Times)**

**CHELSEA YAMFUATA CUBARSI**
CHELSEA bado inamtaka beki Mhispania mwenye umri wa miaka 16, Pau Cubarsi, ambaye ameichezea Timu B ya Barcelona msimu huu. **(Sport)**

**MERJI AGOMBEWA ULAYA**
KIUNGO wa kati wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Tunisia, Hannibal Mejbri mwenye miaka 20 anasakwa na klabu za Freiburg, Lyon na Sevilla. **(Bild)**

**JUVENTUS KUMTOA KEAN**
JUVENTUS iko tayari kumtoa mshambuliaji wa Italia, Moise Kean, mwenye umri wa miaka 23 ili kubadilishana na kiungo wa kati wa Arsenal, Charlie-Michael Patino (20), ambaye yuko Swansea City kwa mkopo. **(Tuttosport)**

**NKETIAH ANUKIA PALACE**
KLABU ya Crystal Palace imekuwa ikimuulizia mshambuliaji wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Eddie Nketiah, mwenye umri wa miaka 24, kwa nia ya kutaka kumnunua**. (Mail)**

**RAMSDAL KUONDOKA ARSENAL**
Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta yuko tayari kuwaruhusu Edie Nketiah, mshambuliaji Emile Smith Rowe mwenye miaka 23, na kipa, Aaron Ramsdale (25), kuondoka iwapo watapokea ofa kubwa. **(Mirror)**

**SPURS, ROMA VITANI**
KLABU ya Tottenham Hotspur inatarajiwa kuongeza juhudi za kutaka kumnunua beki wa Genoa mwenye umri wa miaka 21, Radu Dragusin lakini watakabiliwa na ushindani kutoka kwa Roma.**(Telegraph)**

**BENSEBAINI AITAKA UNITED**
MLINZI wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Algeria, Ramy Bensebaini, mwenye umri wa miaka 28, amesema angependa kujiunga na Manchester United. **(La Gazette du Fennec)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI AAMUA KUIKATAA BRAZIL

## ●●● Ni baada ya kuongeza mkataba wa kubakia Madrid hadi...

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti amekubali kuongeza mkataba wa kuendelea kukinoa kikosi cha Real Madrid hadi Juni, mwaka 2026 na kuitosa ofa ya kuifundisha Timu ya Taifa ya Brazil.

Ancelotti mwenye umri wa miaka 64, alirejea katika klabu hiyo mwaka 2021 kwa kipindi chake cha pili na kushinda mataji mawili ya LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya katika msimu wake wa kwanza.

Mkataba wake wa awali ulitarajiwa kumalizika Juni, mwakani na Mtaliano huyo amekuwa akihusishwa mara kwa mara kuchukua majukumu ya kuinoa Brazil msimu ujao wa joto.

Kwa mujibu wa ESPN mazungumzo juu ya mkataba mpya yaliharakishwa baada ya mazungumzo kufanyika kati ya Ancelotti na Rais wa Real Madrid, Florentino Perez Alhamisi iliyopita.

Ancelotti alieleza masharti yake ya makubaliano -- ikiwa ni pamoja na upendeleo wake klabu isajili beki wa kati katika dirisha la Januari, huku Eder Militao na David Alaba wakiwa nje kwa muda mrefu, na Perez alikubali hilo.

"Real Madrid na Carlo Ancelotti wamekubali kuongeza mkataba wa kocha wetu hadi Juni 30, 2026," klabu hiyo ilisema katika taarifa yake juzi.

"Katika misimu yake mitano kama kocha wa Real Madrid, ameshinda mataji 10: Ligi ya Mabingwa mara mbili, Kombe la Klabu bingwa ya Dunia, Super Cup mara mbili moja la LaLiga, Copas del Rey mbili na Supercopa moja.

Ancelotti ndiye kocha pekee aliyeshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika historia ya mashindano hayo.

Pia ndie kocha mkuu wa kwanza kushinda Ligi Kuuu tano za Ulaya (Italia, England, Ufaransa, Ujerumani na Hispania)

"Leo ni siku ya furaha. Real Madrid na mimi tutaendelea na safari yetu pamoja tukitafuta mafanikio mapya zaidi," aliandika Ancelotti kwenye ukurasa wake wa X.

Ancelotti alikuwa akikabiliwa na maswali ya mara kwa mara kuhusu mustakabali wake kutoka kwa vyombo vya habari msimu huu, huku mkataba wake ukiingia miezi ya mwisho.

Baada ya kuinoa Juventus, AC Milan, Chelsea na Paris Saint-Germain, alijiunga na Madrid kwa mara ya kwanza mnamo 2013, akishinda Ligi ya mabingwa Ulaya na Copa del Rey kabla ya kutimuliwa miaka miwili baadaye.

Alirejea Bernabeu mnamo 2021, baada ya kufundisha Bayern Munich, Napoli na Everton kwa muda.

Msimu wa Madrid wa 2021-22 ulikuwa wa mafanikio makubwa, kushinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa, lakini kampeni iliyofuata ilikuwa na changamoto zaidi, kukosa mataji hayo mawili makuu, ingawa walishinda Copa del Rey.




# ARTETA KUMSAJILI DE LIGT JANUARI

**LONDON, Engand**

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta ameripotiwa kumweka katika orodha ya wachezaji anaowahitaji beki wa Bayern Munich, Matthijs de Ligt. kwenye ripoti ya mastaa ambao anataka wasajiliwe katika dirisha lijalo la majira ya baridi.

Areta ameweka wazi anataka kuboresha eneo lake la ulinzi, ambalo licha ya kufanya vizuri kwa msimu huu bado linaonekana kuhitaji mabadiliko.

De Ligt mwenye umri wa miaka 24 ni mmoja kati ya mastaa walioonyesha kiwango bora kwa msimu huu na inaonekana ni vigumu Bayern Munich kumuuza kutokana na umuhimu wake katika timu hiyo.

Pamoja na Bayern Munich kutoonekana inahitaji kumuuza, kuna uwezekano ikabadilisha uamuzi au timu inayomhitaji itatoa kiasi cha zaidi ya pauni milioni 70.

De Ligt alijiunga na Bayern Munich kwa ada ya uhamisho ya pauni 68 milioni mwaka jana akitokea Juventus, mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika ifikapo mwaka, 2027.

Tangu kuanza kwa msimu huu, nyota huyo amecheza mechi 11 za michuano yote na kufunga bao moja.

# Robertson nje muda mrefu

**LIVERPOOL, England**

MLINZI wa Liverpool, Andy Robertson anatazamiwa kubakia nje ya uwanja kwa muda mrefu zaidi, kwa mujibu wa kocha Jurgen Klopp.

Robertson "hajakaribia hata kidogo" kurejea mazoezini huku akiendelea kupata nafuu kutokana na bega lake lililoteguka alilopata akiwa kwenye majukumu ya kimataifa na Scotland Oktoba.

"Robbo bado anahitaji muda zaidi katika bega lake. Bado hayuko karibu na mazoezi ya timu," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.



"Anaweza kufanya mengi, kila kitu bila kutumia mkono ipasavyo jambo ambalo ni zuri lakini kwa upande mwingine, linaonyesha bado tuna safari ndefu. Kwa hakika nadhani ataikosa Januari yote. Ni lazima afanye hivyo."

Mrithi wa Robertson katika beki ya kushoto, Kostas Tsimikas, pia anatarajiwa kukaa nje ya uwanja kwa muda mrefu baada ya kuvunjika mfupa wa shingo yake kwenye mchezo dhidi ya Arsenal.

Klabu hiyo ina matumaini kuwa kiungo Alexis Mac Allister anaweza kurejea kumenyana na Newcastle Jumatatu huku akiuguza jeraha la goti alilopata dhidi ya Sheffield United mapema mwezi huu.

"Tutazingatia kile anachoweza kufanya, ikiwa anaweza kuingia kwenye mazoezi ya timu au la. Uamuzi haujafanyika, ni mapema sana kwa hivyo tutaona," aliongeza Klopp.

# Martinez aipa ahueni United

**MANCHESTER, England**

MLINZI wa kati wa Manchester United, Lisandro Martinez, ametoa ishara ya taarifa njema kwa mashabiki kwani anatarajia kurudi dimbani hivi karibuni.

Beki huyo anayepigana hajacheza tangu alipouguza jeraha la mguu lakini anakaribia kurejea, huku kocha Erik ten Hag hivi majuzi akifichua kuwa anatarajia kumpigia simu Martinez katikati ya Januari.

Ili kujenga zaidi shauku ya kurejea kwa Martinez, aliviambia vyombo vya habari vya klabu ili kutoa ufahamu kuhusu hali yake ya sasa.

"Sawa, mimi kwa sasa naendelea vizuri na ninaweza kurudi uwanjani hivi karibuni," alisema Martinez

"Rehab yangu inaenda kwa kushangaza, kwa jinsi ninavyotaka, ninahisi nguvu, nikifanya kila kitu sawa.

"Na pia idara ya matibabu, wananitunza kutoka siku ya kwanza, kwa hiyo ilikuwa muhimu sana. Ndio, yote ni sawa kwangu."

Licha ya kutamani kurejea haraka iwezekanavyo, Martinez alikiri umuhimu wa kuwa waangalifu ili kuepuka kufanya madhara yoyote zaidi.

"Hakika tunatakiwa kuwa na subira, tuwe na subira," alisema. "Najua kwamba nitarudi hivi karibuni. Inachukua muda, tunahitaji kuwa na subira."

Akiwa amekosa mwisho wa msimu uliopita kutokana na jeraha kama hilo, Martinez alikiri kwamba amekuwa na shida ya kukaa nje kwa muda mrefu lakini akaelezea jinsi ametumia wakati wake nje ya uwanja kujiboresha.

"Ni ngumu, ngumu sana, haswa ulipokuwa na majeraha mawili, karibu miezi sita au saba, ni ngumu sana," alisema.

"Lakini ninahisi kuwa na nguvu kutoka kwa akili yangu, kutoka kwa familia yangu, kutokukata tamaa, kwa hivyo hii imenifanya kuwa na nguvu zaidi. Ni ngumu, ngumu sana, lakini hakuna visingizio."



## HABARI MICHEZO

# DK. MWINYI AFUNGUKA UJENZI VIWANJA VYA KISASA KUENDELEA

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema haipendezi kuona ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi, vijana wanacheza mpira kwenye viwanja vyenye vumbi na kuongeza wakati umefika sasa wa kujenga viwanja vya michezo vya kisasa ambavyo vitakidhi viwango vya kimataifa.

Dk. Mwinyi amesema hayo wakati akifungua viwanja jumuishi vya kisasa vya michezo vinavyojulikana kwa jina la Matumbaku Sports Complex vilivyoko katika Jimbo la Kikwajuni ambavyo vimejengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF).

Alisema serikali yake imeamua kufanya jitihada maalum za kuimarisha miundombinu ya michezo ili kukuza vipaji vya vijana katika aina zote za michezo.

"Ndiyo maana tumekuja na utaratibu huu mpya wa kujenga viwanja vya michezo vya kisasa na tumekuwa tukihamasisha wawekezaji mbalimbali," alisema Dk. Mwinyi.

Aliongeza serikali inafanya hayo yote ili kuendeleza michezo kwa kujenga miundombinu iliyo bora na imara na hivyo vijana kupata nafasi ya kuonyesha vipaji vyao.

Alisema pia hatua hiyo itaziwezesha taasisi zinazohusika na michezo kuibua vipaji hivyo na kuvitumia katika kuitangaza nchi katika mashindano ya kitaifa na kimataifa.

"Kama inavyojulikana michezo nayo ni ajira, hivyo serikali inatilia mkazo ujenzi wa viwanja vya michezo mbalimbali ili kutanua wigo wa ajira kutokana na michezo,"alisema kiongozi huyo.


Hata hivyo Dk. Mwinyi alisema soko la ajira zinazotokana na michezo linakua kila kukicha na kufungua mipaka hadi kufikia katika maeneo ya mbalimbali ya dunia.

Alisema pia michezo ikitumika vizuri itakuwa ni moja kati ya njia ya kuitangaza Zanzibar na kukuza utalii ambao kwa kiasi kikubwa unachangia mapato ya nchi na kukuza uchumi wake.

"Jambo la kwanza ni hatua ambayo Tanzania imefikia kimichezo na hasa mpira wa miguu. Kupitia timu zetu kubwa za Yanga na Simba, katika michezo ya Klabu Bingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, na kupelekea hata ufunguzi wa mashindano ya Ligi ya Afrika kufanyika Tanzania na kuhudhuriwa na Rais wa FIFA na Rais wa CAF," kiongozi huyo alisema.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZSSF, Nassor Shaaban Ameir, alisema kuna ushirikiano mzuri na Wizara ya Fedha katika kuhakikisha wanasimamia agizo alilolitoa Dk. Mwinyi juu ya kuukamilisha ujenzi wa uwanja huo.

Ameir alisema uwanja huo wa kisasa unatambulika rasmi kwa sababu umekidhi mahitaji yote ambayo yalitakiwa kutekelezwa.




Mshindi wa Promosheni ya Magifti Dabodabo, Loveness Hidana (kulia) akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni tano kutoka kwa Meneja Mauzo wa Kampuni ya Tigo Mkoa wa Kilimanjaro, Silas Mkuyu, baada ya kuibuka mshindi katika promosheni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zahera ateuliwa kuinoa Namungo

**Na Adam Fungamwango**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Yanga, Polisi Tanzania na Coastal Union, Mwinyi Zahera, ametangazwa rasmi kocha mpya wa Namungo FC ya mkoani Lindi.

Zahera amechukua mikoba iliyoachwa na Cedriz Kaze, ambaye aliamua kuachana na Namungo baada ya kupata matokeo yasiyoridhisha.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana imesema kwa sasa Namungo itakuwa chini ya kocha huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

"Tunayofuraha kumtambulisha rasmi Kocha Mkuu mpya wa timu yetu, Mwinyi Zahera. Karibu kwenye familia ya Wauaji wa Kusini," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Zahera amejiunga na Namungo akitokea Coastal Union, ambapo alikuwa Mkuu wa Programu za Vijana.

Zahera alitua nchini na kujiunga na Yanga mwaka 2021, na alipotoka katika klabu hiyo alichukuliwa na Polisi Tanzania mwishoni mwaka jana hadi Julai mwaka huu alipojiunga na Coastal Union lakini kutokana na matokeo mabovu alibadilishiwa majukumu.

## Simba SC yamfuata Malonga Brazaville

INATOKA UK. 24

taba na Al Hilal ya Sudan.

"Inaonekana kocha amewaambia viongozi waachane na hao wote, badala yake wamelete haraka Malonga kwa sababu mbalimbali, ikiwamo umri wake pamoja na uwezo wa kucheza namba zaidi ya tatu uwanjani," kilisema chanzo chetu.

Awali Simba ilianza kumfuatilia Modiba mwenye umri wa miaka 28, lakini ugumu ulibakia kwa Mamelodi Sondowns lakini pia kwa mchezaji mwenyewe alihitaji kulipwa mshahara mkubwa ambao viongozi hawakuafiki na nguvu zikaelekezwa kwa Imoro ambaye kocha hajamkubali.

Menaja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alipoulizwa kuhusu usajili wa nyota hao alisema ni kweli wanafanya usajili lakini kwa sasa hawapo tayari kuweka bayana majina mpaka pale muda sahihi utakapofika.

## Taifa Stars, Misri kupimana ubavu

INATOKA UK. 24

mazuri na ndio tutachokidai kutoka kwake, ili timu ikishindwa ndio tumlaumu kocha kwa sababu ana uwezo wa kutueleza lolote," alisisitiza Ndumbaro.

Aliongeza msafara wa Stars kuelekea Misri utakuwa na wachezaji 30 na baadaye watachujwa na kubakia nyota 25 ambao wataenda Ivory Coast kwa ajili ya kupeperusha bendera ya nchi kwenye fainali za AFCON.

Alisema Stars ikiwa kambini Misri, itacheza mechi tatu za kirafiki za kimataifa ikiwamo dhidi ya wenyeji Misri.

Waziri huyo alisema bado mechi nyingine mbili hazijajulikana zitakuwa dhidi ya timu zipi, itakapokuwa tayari itawekwa wazi.

"Tupo Kundi F lenye Morocco, DR Congo, Zambia na sisi Watanzania, sio kundi jepesi, tunaanza na Morocco ukitaka kufanikiwa lazima umfunge bingwa, tunaenda Ivory Coast kupambana kupata matokeo mazuri.

Baada ya mchezo huo tutakuwa na dabi mbili dhidi ya ndugu zetu DR Congo ni Lake Tanganyika na mechi nyingine na Zambia ambao ni TAZARA, Serikali, TFF na benchi la ufundi limejipanga vizuri kwa fainali hizi, kocha ametueleza tunaenda kushindana," Ndumbaro aliongeza.

Alisema serikali ina mchango mkubwa lakini anawaomba mashabiki waendelee kuisapoti timu na hamasa ya safari hii iwe ya juu katika kila mechi ya AFCON kuvaa jezi lakini kutumia mitandao ya kijamii kuizungumzia Stars.

Alisema pia Wizara kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limeandaa harambee itakayofanyika Januari 10, mwakani ili kuchangisha fedha zitakazosaidia Stars na Twiga Stars ambayo baadaye mwakani itakwenda Morocco kushiriki fainali za WAFCON.

Michezo
Jumapili Desemba 31, 2023
Nipashe



## Ancelotti aamua kuikataa Brazil

UKURASA 21



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akikata utepe kuzindua uwanja wa michezo wa Matumbaku Sports Complex uliopo Shehia ya Miembeni Mkoa wa Mjini Magharibi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# SIMBA SC YAMFUATA MALONGA BRAZAVILLE

●●● Yanga kamili kuivaa Jamhuri katika Kombe la Mapinduzi...

**Adam Fungamwango na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI Yanga inatarajia kuanza kampeni ya kuwania Kombe la Mapinduzi leo kwa kucheza dhidi ya Jamhuri, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amewataka mabosi wa timu hiyo kumsajili beki, Hernest Malonga kutoka CSMD Diables Noirs ya Congo Brazaville.

Kuelekea mechi ya leo, Meneja wa Yanga, Walter Harrison, amesema maandalizi ya kikosi chake yamekamilika na wako tayari kuwapa burudani mashabiki wao.

Meneja huyo alisema wanahitaji kufanya vizuri katika mashindano hayo, hivyo watatumia wachezaji wote waliobakia baada ya nyota wake wengine kuitwa kwenye timu za taifa.

"Ni mechi ambayo haitakuwa nyepesi, wapinzani wetu wamejipanga kusaka ushindi na sisi pia tunazitaka hizo alama tatu, tumekuja kamili kupambana na si kusindikiza," alisema meneja huyo.

Kocha Mkuu wa Jamhuri, Mohamed Mtumwa, alisema timu yake ina wachezaji wenye uzoefu wa kucheza na Yanga kutokana na kukutana nayo mara kadhaa katika mashindano hayo.

Mtumwa alisema hawana hofu yoyote na mechi hiyo na malengo yao ni kumaliza 'uteja' dhidi ya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema benchi la ufundi limezungumza na wachezaji kwa ajili ya kuwajenga kisaikolojia ili kutowaogopa wapinzani wao na kuondoa dhana ya kufungwa kabla ya mchezo.

"Tumewatoa hofu wachezaji wetu kuelekea mchezo wetu wa pili ambao huu ndio utakaotupa mwanga wa kusonga mbele katika michuano ya mwaka huu iwapo tutashinda, hivyo wajue kama tunacheza na timu kubwa ni suala la umakini na kutokuwa na pupa ya mchezo, hii ndilo linahitajika," Mtumwa alisema.

Mechi nyingine ya mashindano hayo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Jamus FC kutoka Sudani Kusini dhidi ya KVZ FC, itakayofanyika kuanzia saa 10:15 kwenye Uwanja wa Amaan.

Kocha Mkuu wa Jamus, John Alier, alisema ingawa ni mara ya kwanza kushiriki michuano hii lakini mipango yao ipo vyema kuhakikisha wanaonyesha ushindani.

Alier alisema anajua michuano hii ni migumu kwa sababu inashirikisha timu zenye uzoefu wa michuano mbalimbali ya kimataifa.

"Ni mara yetu ya kwanza kushiriki michuano hii, malengo yetu makubwa ni kuhakikisha tunashinda michezo yetu yote ili tutimize lengo kuu la kunyakua ubingwa," aliongeza kocha huyo.

Taarifa kutoka Simba zinasema Benchikha anamhitaji Malonga ili kuchukua nafasi ya Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' huku pia wakipanga kufanya mazungumzo na mabeki wengine wawili kutoka nje ya Tanzania.

Nyota ambao watanajwa majina yao yako mezani ni mabeki wa kushoto, Aubrey Modiba wa Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini na Ibrahim Imoro aliyemaliza mka-

INAENDELEA UK 23

## Taifa Stars, Misri kupimana ubavu

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Dk. Damas Ndumbaro, amewataka wadau wa soka nchini kumwacha Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Adel Amrouche, kuwatumia nyota wanaocheza kandanda nje ya Tanzania na endapo watafanya vibaya ndio alaumiwe.

Ndumbaro alisema kocha anatakiwa kufanya majukumu yake kwa uhuru ambao anaamini wataipeperusha vyema bendera ya Tanzania katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), zitakazofanyika mapema mwakani nchini Ivory Coast.

Alisema kikosi cha Stars ambacho kipo Zanzibar kitakwenda kuweka kambi yake Misri kati ya kesho na keshokutwa na kitakaa huko hadi Januari 8, mwakani na kuanza safari ya kuelekea Ivory Coast katika fainali hizo.

"Ukiangalia vizuri utabaini Tanzania tumebarikiwa wachezaji wengi katika mataifa mbalimbali ila tunawaomba Watanzania kumpa nafasi kocha Adel kufanya majukumu yake.

Tunatakiwa kumpa nafasi kufanya mipango yake na kusubiri matokeo

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >